*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 6 Septemba, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa maswali, swali letu leo la kwanza ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na.30

**Mkakati wa Kumaliza Ugonjwa wa UKIMWI**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza ugonjwa wa UKIMWI kufikia mwaka 2030 kama Azimio la Umoja wa Mataifa linavyoelekeza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumaliza ugonjwa wa UKIMWI ifikapo mwaka 2030 kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Mataifa, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

Moja, ni kuendelea kutekeleza mkakati wa nne wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI Tanzania wa mwaka 2018 mpaka 2023. Mkakati huu umeainisha maeneo saba ya kimkakati yatayowezesha kufikia malengo ya sirufi tatu ikiwa ni ya kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kuendelea kuratibu mipango ya sekta zote katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Pili, kuhamasisha upatikanaji na utumiaji wa kondomu; tatu, kutokomeza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, nne, kuendeleza tohara ya hiari ya kitabibu kwa wanaume kwenye mikoa yenye kiwango kidogo cha tohara; tano, kinga ya tiba, matumizi sahihi na endelevu ya *ARV's* na sita ni mkakati wa kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kwenye makundi yaliyo katika hatari ya kuambukizwa. Makundi haya ni pamoja na wasichina balehe na wanawake vijana, wanaojidunga dawa za kulevya, wasichana wanaouza ngono, wafungwa, wavuvi, wachimbaji wa madini kwenye migodi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuendeleza usimamizi wa Mfuko wa Dhamana wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund)* ili kuimarisha ukusanyaji wa rasilimali fedha na nyingine kupitia vyanzo vya ndani vya nchi ikiwa ni jitihada za kupunguza utegemezi wa fedha za wafadhili nje. Tatu, kurekebisha Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001 pamoja na sera nyingine husika. Vilevile sheria mbalimbali ili zitoe miongozo ya programu na mifumo ya kudhibiti maambukizi mapya ya UKIMWI nchini. Na mwisho ni kuhamasisha wanaume kupima VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa UKIMWI ni janga linalotukabili zote kama Taifa. Hivyo sisi tukiwa kama wawakilishi wa wananchi tunao wajibu wa kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika kupunguza na hatimaye kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, stadi zinaonesha lipo jaribio linalohusisha utolewaji ama utumiaji wa *ARV* kwa watu wasio kuwa na maambukizi ya VVU ama UKIMWI ikiwa ni njia mojawapo ya kuzuia maambukizi mapya endapo mtu huyu aliyetumia *ARV* pasipo kujamiana na mtu ambaye tayari ana maambuki ya VVU ama UKIMWI.

Ningependa kusikia kauli ya Serikali hali ipoje nchini Tanzania juu ya matumizi hayo ya *ARV* kwa mtu ambaye hana maambukizi ili kumzuia asiambukizwe endapo atajaamiana na mtu mwenye maambukizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kufuatia mikakati inayofanywa na Serikali ambayo mengi wameainisha kwenye majibu yao ningependa kujua jambo moja mahususi. Je, Serikali inashughulikiaje swala zima la ongezeko la watoro ambao tayari wako kwenye kujiunga na utumiaji wa matibabu ya *HIV and AIDS?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri mhusika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi katika matibabu ya ugonjwa wa UKIMWI yameonesha

kwamba mtu asiyekuwa na maambukizi ya UKIMWI anaweza akapatiwa dawa ambazo zinaweza kumsadia kumkinga dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa lugha ya kitaalamu inaitwa *pre-exposure prophylaxis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuweke msisitizo hadi hivi sasa hatuna tiba ya ugonjwa wa UKIMWI, tunachokifanya hichi ni dawa kinga, na sisi kama Tanzania tunalitambua hilo na tumeshaanza katika ngazi ya majaribio na lengo letu ni kwamba baada ya majaribio haya tuweze *roll out* nchi nzima na tunalenga makundi mahususi ambayo ni pamoja na wanaofanya biashara ya ukahaba, kwa wale ambao wanajidunga madawa ya kulevya na wale ambao wanajamiiana kwa jinsia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kwamba kinga hii inaendana sambamba na kutumia njia nyingine za kujikinga na wala sio suluhu ya kutopata maambuzi ya UKIMWI, niliutaka niliweke msisitizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana wale ambao wanaacha dawa.

Sasa hivi Serikali tumeanza mchakato wa kuwabaini na changamoto ambayo tumeiona ni kwamba siyo kwamba wengi wanaacha ni mtu amekuwa eneo moja anachukua dawa baada ya hapo anahamia katika nyingine na kule anaenda kujisajili kama mteja mpya na sisi tumekuwa hatuna kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tuna kitu ambacho tunachokifanya ni kuweka utaratibu wa kutumia mifumo wa *biometric* kwamba mtu akipata matibabu sehemu moja akienda tena sehemu nyingine atatambulika kama ni mtu ambaye tayari tunaye kwenye *database* na hili tunalifanyia kazi na hivi karibuni tutali-*introduce. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kinipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya njia ya kupunguza maambukizi ya UKIMWI ni kuhakikisha kwamba vituo vya utoaji wa huduma vinakuwa jirani na wananchi. Kwenye maeneo ya vijijini vituo vya afya vipo mbali na zahanati maeneo mengi hazitoi huduma hizi za kupima,lakini pia utoaji wa dawa.

Je, ni lini Serikali itaagiza au itaweka utaratibu rasmi kuhakikisha kwamba vituo vya afya na zahanati zote zinatoa huduma ya upimaji, lakini pia zinatoa huduma za *ARV?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, Mheshimiwa Waziri mhusika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Hongoli. Sisi kama Serikali mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba ifikapo 2030 tumeweza kufikia asilimia 90 ya Watanzania tunaowapima, asilimia 90 ya wale ambao tumewapima tunawaanzishia dawa na asilimia 90 ya wale ambao tumewaanzishia dawa tuweze kufubaza virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ambayo tumekuja nayo tumeendelea kupanua wigo wa vituo vyetu vya kutolea huduma hizi za ugonjwa wa UKIMWI. Lakini tumeanzisha mkakati wa kuwa na kitu kinaitwa *outreach,* watoa huduma wetu wa afya kwenda kule katika maeneo ambapo hakuna huduma za kuweza kuweza kutoa huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaendelea kuhamasisha Watanzania kwa utaratibu ambao tunaenda nao sasa badala ya kutoa dawa za mwezi mmoja mmoja tumeongeza sasa tu kwa wale wagonjwa ambao wako *stable* sasa hivi tunatoa dawa za miezi mitatu mitatu na yote haya ni mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba

huduma hizi zinawafikia wananchi wengi iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa mwenyekiti, nakushukuru sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kujua tu kwamba sasahivi wananchi wengi wameshaelimika kuhusiana na masuala ya UKIMWI. Lakini nilitaka Serikali ituambie ni kwa nini hawaruhusu watu wajipime wenyewe kwa *rapid* ya *HIV test* kwa sababu wakienda vituo vya afya usiku vinakuwa vimefungwa na kuna watu wanapenda kufanya hilo jambo kwa *chap chap.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wasiruhusiwe wapate hivi vipimo waweze kujipima ili waende kwenye hiyo shughuli wakijua wako salama au hawako salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri kubwa lao.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya UKIMWI, upimaji unafanyika katika kituo cha afya. Lakini tumeanza mchakato ndani ya Serikali ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI ili sasa watu waweze kujipima wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kumeibuka mjadala kuna wengine wanasema mtu akijipima mwenyewe atakuwa *frustrated* ataenda kuambukiza wengine. Kwa hiyo, tunaweka kwamba tutaanza ajipime mwenyewe mbele ya mtoa huduma za afya. Hayo ndiyo mapendekezo ambayo tumeyatoa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tutakuja Bungeni tuwaombe Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Chumi.

Na. 31

## Fedha Zinazotoka kwa Mataifa Yanayoharibu Mazingira

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Mataifa makubwa duniani yanayoongoza kwa kuharibu mazingira, kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa na mifuko kama vile *Climate Investment Funds (CIF), Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF)* na kadhalika wamekuwa wakitenga fedha kwa ajili ya kusaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Je, Taifa limejipangaje kunufaika na fedha za mifuko hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niombe radhi kwa sauti, lakini pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako tukufu naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimshukuru Makamu wa Rais Mama yetu mama Samia Suhulu na wafanya kazi wote wa Ofisi yetu ya Wizara yetu kwa ushirikiano mkubwa wanaouonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri Mkuu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano mkubwa ambao anauonesha kwetu. Lakini nisisahau kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Singida Mjini pamoja na familia yangu kwa ushirikiano wanaouonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya shukrani hizo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira nijibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza kunufaika na fedha kutoka katika Mifuko ya Kitaifa ya Mabadiliko ya tabianchi, Serikali imejipanga kwa kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2012 na inakamilisha Mpango wa Taifa wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kukamilika kwa mkakati huo kwa mpango huo utaiwezesha nchi kunufaika na fedha kutoka mifuko hiyo. Mkakati wa mpango huo umeainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya kuandaa miradi ya kukabiliana na mabaliko ya tabianchi ambayo imeombewa fedha na utekelezaji kutoka katika mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania tayari imeanza kunufaika na fedha za mifuko hiyo kupitia mfuko wa *GEF*, tunatekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na miradi ya kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame ya Tanzania ambapo tumepata dola za Kimarekani 7,155,963 na mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupitia mfumo ikolojia katika maeneo ya vijiji nchini Tanzania tuliopata dola za Kimarekani 7,571,233.

Aidha, kwenye mfuko wa *GEF* katika mzunguko wake wa sita zilitengwa dola za Kimarekani milioni mbili ambazo zinatumika kwa ajili ya kutekeleza miradi midogo midogo ya nchi. Mfuko wa *GCF* ulianzishwa mwaka 2011 na ulianza kutoa fedha mwaka 2015. Kwenye mfuko huo Tanzania ilitarajia kupata dola za Kimarekani 124 kwa ajili ya mradi wa maji wa Simiyu unaotekelezwa chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Tanzania inakamilisha utaratibu wa kupata dola za Kimarekani 300,000 kutoka *GCF;*

ambazo zinatumika kujenga uwezo kwa Taasisi zetu ili ziweze kuandaa miradi itakayofadhiliwa na mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Climate Investment Fund* inajumuisha mifuko miwili iliyoanzishwa mwaka 2008, mifuko hiyo ni *Clean Technology Fund* na *Strategic Climate Fund*. Mdhamini wa mifuko hii ni Benki ya Dunia, mifuko hii hutoa mikopo yenye riba nafuu kwa nchi zinazoendelea na kwa ajili kutekeleza miradi ya kupunguza uzalishaji wa gesi joto ambayo siyo kipaumbele cha nchi za Afrika ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kukuza uelewa na kuhamasisha sekta mbalimbali kutekeleza mkakati wa mabadiliko ya tabianchi kwa kuandaa miradi ambayo inakidhi vigezo vya vifuko hii ili Taifa liendelee kunufaika na fedha hizi. Aidha, Serikali kupitia taasisi zake mbalimbali imefanya tijihada za kujisajili yaani *accreditation* na Mfuko wa Mabadiliko wa Tabianchi ili taasisi hizi ziweze kuwasilisha maombi ya fedha hizo moja kwa moja kutoka mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na maelezo hayo mazuri na jitihada hizo za Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza ninaona hapa ni mamilioni mengi sana yamekuja katika nchi yetu ninauliza Serikali. Je, ni lini maeneo mahususi kama ya Mufindi, Njombe na Ruvuma ambako wananchi wana mwamko wa hali ya juu katika kupanda miti ambayo inasaidia kwa kiasi kikubwa ku-*regulate* mambo ya tabianchi. Lini wananchi hawa nao wataanza kunufaika na fedha hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili umeeleza kuhusu *accreditation,* kati ya tatizo kubwa ambalo linasababisha

Taasisi zetu hapa nchini hususani za kijamii kama *NGO's* kukosa fedha kutoka mifuko hii ni kwa sababu sisi kama Taifa bado hatujafanya *accreditation* katika huo mfuko ambao umeutaja.

Je, ni lini Serikali itakamilisha utaratibu huo ili pamoja na fedha hizi ambazo Serikali inazipata moja kwa moja taasisi pia za kiraia kama ma *NGO's* yanayojishughulisha na mazingira yaweze pia kuanza kunufaika na fedha hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi ametaka kujua ni lini fedha hizi zina tutazipata ama tutaweza kuzitumia hasa kwa watu ambao wanawajibika na suala la kutunza mazingira kwa kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Chumi kwamba kwa sababu sisi *focal point,* sisi ndiyo waratibu wa mifuko hii hasa *GEF,* kwa hiyo wakati wowote tutakapokuwa tumepata fedha hizi hasa *GEF7* maana yake tutatangaza ili kuhakikisha kwamba tunaweka vipaumbele kwenye eneo hili la wenzetu ambao wanashughulisha kutusaidia kwa ajili ya kutunza mazingira kwa kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia *NGO's* na tuliposema kuhusiana *accreditation* maana yake tunatarajia fedha zitakapokuja tutaweka bayana na *NGO's* zote na vikundi vyote ambavyo vimesajiliwa vipata fursa ya kuomba fedha hizo na sisi tutawapa kipaumbele, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM. HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri katika nchi yetu kuna mazoea ya kwamba miradi hii ya hifadhi

ya mazingira inafadhiliwa fedha nyingi kutoka kwa wafadhili lakini wanapoondoka tu miradi yenyewe inakufa kwa mfano HADO, HASHI, katika ile miaka ya mwishoni mwaka miaka ya 1980.

Je, Mheshimiwa Waziri unatuhakikishiaje fedha hizi zitakazokuja sasa kwa ajili kukabiliana na tatizo la tabianchi zitatumika vizuri na zitakuwa endelevu ili kukidhi kile kiwango cha kupotea kwa misitu ya hekta laki 350,000 kila mwaka katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumeanza utaratibu wa kuwashirikisha wananchi moja kwa moja katika miradi yote ambayo inakuja na miradi hii wananchi wenyewe wanatengeneza utaratibu wa kuweza kusimamia. Kwa hiyo, ni imani yetu kwa kupitia watalaam wetu na wananchi kuwashirikisha moja kwa moja na nimuombe Mheshimiwa Mbunge na yeye awe sehemu ya kuhakikisha kwamba hili suala linakuwa endelevu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Na Wakuu wa Mikoa na ma-*DC* iwe ni ajenda maalum ya mazingira katika maeneo yao. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro inategemea sana upandaji miti wa wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro na unyevunyevu wa ile miti ndiyo unasaidia theluji mlimani iweze kuendelea kukaa na ikae kwa muda mrefu. Sasa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri au Serikali, fedha hizi zitakapopatikana maeneo muhimu kama haya yenye Hifadhi za Taifa kama mlima wetu, mko tayari hizi fedha zisaidie wananchi wale ili waweze kupanda miti kwa wingi kwa ajili ya kuhifadhi theluji katika ule mlima wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mko tayari kutoa pesa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ni kwamba tuko tayari kutoa fedha kwa kushirikiana pia na wezentu wa Maliasili hasa Wakala wa Misitu ambao pia watatusaidia kupata miti inayoweza kuhimili maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali lako la kwanza umejibu vizuri hongera sana Waziri. Mheshimiwa Gekul.

Na. 32

**Magugu Maji Katika Ziwa Babati**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Ziwa Babati limejaa magugu maji na Halmashauri haina bajeti ya kusafisha ziwa hilo kwa maana ya kuondoa magugu hayo. Je, ni lini Serikali itasaidia kuondoa magugu hayo ili kulinusuru ziwa hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Babati Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, magugu maji ni moja ya viumbe vamizi wageni *(Invasive Alien Species)* ambayo ni moja ya changamoto kubwa inayokabili mazingira yetu nchini. Baadhi ya maeneo yaliyoathirika na mimea ya aina hi ni pamoja na Ziwa Jipe, Ziwa Victoria, Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro. Athari za mimea vamizi wageni kama magugu maji ni kusambaa kwa kasi katika eneo lilivamiwa pamoja na kusababaisha kutoweka kwa baionuai asili katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kubaliana na tatizo hili, nchini Ofisi ya Makamu wa Rais imeitisha mkutano wa wadau uliofanyika terehe 4 Septemba, 2018 ili kushirikiana na wadau katika kutafuta ufumbuzi wa kukabiliana na tatizo hili kitaifa ikiwa ni pamoja na Ziwa Babati. Mkakati huu utakuwa ni muendelezo wa mkakati wa Kitaifa wa kuhifadhi mazingira ya pwani, bahari, maziwa, miti, mabwawa wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huo wa wadau umeandaa mapendekezo ya hatua za kuchukua kitaifa kukabiliana na nchangamoto za uharibinfu wa mazingira unaotokana na mmea vamizi wageni katika magugu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua juhudu za Halmashauri ya Babati na Bonde la Maji la Kati ambapo imeandaa andiko la mradi unaoihusu uhifadhi wa mfumo wa ikolojia wa Ziwa Manyara ambapo Ziwa Babati ni moja ya sehemu ya mfumo wa ikolojia hiyo. Katika andiko hilo, uondoaji wa magugu maji katika Ziwa Babati ni moja ya shughuli za mradi huo. Serikali inaendelea na utaratibu stahiki kuwashirikisha washirika wa maendeleo kupata fedha za kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi izngine zilizochukuliwa na Halmshauri ya Mji wa Babati ni pamoja na kuweka mabango ya makatazo ya shughuli za binadamu ndani ya mita 60 ya eneo la ziwa. Mabango 20 yaliwekwa maeneo yaliyozunguka Ziwa Babati, kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira na kuhimiza kilimo cha makingamaji katika maeneo ya Kata za Bagala, Babati, Mangala, Singe na Bonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhibiti shughuli za kilimo na ufugaji katika eneo la Ziwa Babati na vilevile Halmashauri ya Mji wa Babati imepata Muwekezaji wa shughuli za kitalii karibu na eneo la Ziwa Babati na moja ya makubaliano ni kuondoa magugu maji katika eneo la ziwa hilo. Taratibu za kufikia makubaliano zinaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais itashirikiana na Halmashauri husika kwa kutoa wataalam wakati wa kuondoa magugu maji katika ziwa hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza naomba tu nimsahihishe Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tuna Kata ya Nangara na siyo Mangara lakini pia tuna Kata ya Bagara siyo Bagala, kwa hiyo nafikiri uta-*capture* hayo msahihisho. Naomba niulize maswali haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa mara ya kwanza niko *disappointed* kwa mara ya kwanza, hii ni *essay* siyo majibu na umenikumbusha wakti nipo Chuo Kikuu nilikuwa nikikosa jibu naandika *the whole topic* kama ni *democracy and election* naandika...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali lako, Mheshimiwa Gekul nenda kwenye swali. Kama hujaridhika na majibu ziko taratibu za kumfuata Waziri siyo hivi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea...

**MWENYEKITI:** ...uliza swali lako una maswali mawili.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri haya uliyoandika ya Ziwa Jipe umeanzia Kenya, ukaja Ziwa Manyara kwanza lipo Mto wa Mbu hili andiko la Ziwa Manyara wala halihusiani na Babati na hakuna ulichojibu naomba sasa nikushauri; ni kwa nini usiongee na watu wa *TANAPA* watoe fedha, wasafishe Ziwa Babati kwa sababu sisi tuliomba mtupatie fedha wewe hapa hujasema unatupa fedha.

Sisi tunawalindia viboko wao, wanaua watu wetu, hakuna fidia basi nenda *TANAPA* wakupe fedha tusafishe Ziwa Babati *otherwise* msituachie Halmashauri sisi hatuna vyanzo hata ushauri huo naamini unaupokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. *Infact* katoa ushauri hana hata swali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea ushauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara kwa hatua inayochukua. Tatizo linaloikumba Ziwa Babati kadhalika linaikumba Ziwa Tawi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na kwa kuwa tatizo hili ni tatizo mtambuka kwa nchi nzima.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuunda wataalam kwa nchi nzima na baadae kuzitafutia fedha za kunusuru maziwa hayo ili yaweze kuendelea kutoa huduma kwa jamii na viumbe wengine hai?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu kwenye swali la msingi nimeeleza tarehe 4 Septemba kimefanyika kikao cha wadau ambapo Waziri alikuwa amekisimamia na moja ya mambo ambayo wamejadili ni mkakati wa kuhakikisha kwamba wanaondokana na tatizo hili la magugu maji.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu huu tutaendelea nao na baada ya kuweka ule mkakati basi tutahakikisha kwamba tunaweza kuondoa tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali na Mheshimiwa George Lubeleje.

Na. 33

**Kuhamisha Reli Kuanzia Kidete - Godegode - Gulwe**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Stesheni ya treni ya Kidete - Godegode - Gulwe na Msagali treni hukwama mara kwa mara kutokana na mafuriko wakati wa mvua na Serikali ina mpango wa kujenga reli ya *standard gauge* kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamisha reli hiyo kuanzia Stesheni ya Kidete - Godegode - Gulwe mpaka Msagali na kupitisha eneo lingine ambalo hakuna mafuriko ili kuondoa usumbufu wa abiria ambao hukaa maeneo hayo treni inapokwama au reli inapochukuliwa na mafuriko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seneta George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mafuriko katika eneo hili ni la muda mrefu na Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi za kukabiliana na changamoto hii zikiwemo ujenzi wa mabwawa pamoja na kuendelea kutafuta fedha kutoka taasisi mbalimbali za kifedha kwa ajili ya ujenzi wa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la *JICA* tayari limekwishakamilisha upembuzi yakinifu kuhusu upatikanaji wa suluhisho la kudumu katika eneo hilo. Aidha, mazungumzo baina ya Serikali yetu na Serikali ya Japan

yanaendelea ili kupata fedha kwa ajili ya kutatua tatizo hili la mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ili kuepukana na uharibifu unaojirudia kila mwaka kutokana na mafuriko, yafuatayo yanafanyika katika ujenzi wa reli mpya ya *standard gauge:-*

(i) Reli mpya haitokuwa karibu na mito na kuipitisha vilimani zaidi ya kingo za Mito ya Mkondoa na Chinyasungwi na kuna maeneo korofi ambapo reli itakuwa zaidi ya kilometa mbili kutoka reli ya sasa ilipo.

(ii) Reli itajengwa ndani ya mahandaki yaani *tunnels* na madaraja yenye mihimili iliyoinuliwa juu zaidi. Kwa kuzingatia utatuzi huu, kutajengwa mahandaki manne yatakayokuwa na umbali wa jumla ya kilometa 2.75 pamoja na madaraja yenye uwazi yaani *span* ya mita 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wnanachi wanaoishi jirani na reli zetu wazingatie na kuheshimu eneo la njia za reli kuepuka uharibifu wa reli zetu ambazo zinagharimu pesa nyingi kuzirekebisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza katika majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba watajitahidi kukwepa hii reli mpya watakwepa Mto Mkondoa na Mto Kinyasungwi na hii mito ndiyo yenye maji mengi yanayosababisha mafuriko maeneo ya Gulwe mpaka Godegode.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, kwa kuwa maji haya huwa yanasambaa kilometa tatu na yeye anasema atajenga kukwepa kilometa mbili, Je, itawezekana? Mafuriko siyataendelea na reli itaharibika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili; eneo la Gulwe kuna makorongo makubwa sana. Mwaka 1996 tulipata mtaalam Johnson kutoka Marekani alijenga ma-*gabion* makubwa sana lakini mvua moja tu ma-*gabion* yote yalikwenda. Sasa una maelezo gani Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa jinsi anavyofuatilia na mara kadhaa amekuwa akifika hata ofisini kwa ajili ya kuangalia kwamba eneo lenye matatizo ya mafuriko ya mara kwa mara linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumtaarifu tu kwamba ni kweli maji huwa yanasambaa mpaka kilometa moja, lakini kama atavuta kumbukumbu vizuri mwezi wa pili mwishoni nilitembelea eneo la mafuriko na nikatoa maagizo kwa Mkuu wa Wilaya wa eneo hilo pamoja na kuwasihi wananchi kwamba eneo la reli kwa upande ule ni mita 60 kwa upande wa kushoto na mita 60 upande wa kulia, hawatakiwi wafanye shughuli zozote za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za kibinadamu ni moja kati ya sababu kubwa zinzosababisha reli yetu kufurikishwa na maji kwa sababu ukishaanza kulima kando kando ya reli unasababisha ule udongo unakuwa tifutifu, ukisababisha udongo kuwa tifutifu maji yakija ni lazima yatabomoa ile reli, lakini kama hakuna shughuli za kibinadamu maana yake ile miti itaendelea kuota na kuzuia. Ile reli haikujengwa kwa bahati mbaya, ilifanyika utafiti ndiyo ikajengwa maeneo yale, lakini niendele kutoa msisitizo kwa wananchi kwamba wasivamie maeneo ya reli na wakae mbali mita 60 kutoka kwenye reli ilipo upande wa kushoto na kulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili; ni kweli kwamba hiyo *gabion* ilijengwa kubwa na kutatua hilo ni ile njia yetu ya pili kwamba reli itajengwa ndani ya mahandaki mbali kilometa mbili kutoka reli ilipo. Tutajenga *meter gauge* pamoja na *standard gauge* ili kuhakikisha kwamba hayo maji sasa hayaji na wananchi tuna uhakika hawatakuja kutuvamia kule kwenye milima ambapo tunajenga reli yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndumbaro.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza; Makao Makuu ya Shirika la Reli Tanzania pale Dar es Salaam hasa Ofisi ambako wanachapisha tiketi za Nchi nzima jengo lile lipo kwenye hali mabaya mno.

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu sasa wa kulikarabati jengo lile ili wafanyakazi wanaofanyakazi mle ndani na wao wajione ni sehemu ya matunda ya Taifa hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, wajiandae Mheshimiwa Ndumbaro na Mheshimiwa Frank.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba jengo la Makao Makuu wa Shirika la Reli Tanzania pale Dar es Salaam linahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge siyo jengo lile tu peke yake, ni majengo mengi sana ya vituo vya Mikoa ambayo kwa kweli hali zake ziyo nzuri na kupitia Shirika la Reli Tanzania tumekwishatoa maelekezo kama Serikali wapitie maeneo yote yale na sasa hivi kuna timu ya wataalam ambao wanapitia kila eneo la majengo ya reli na kuhakikisha kwamba wanaleta gharama nzima pamoja na vile vituo ambavyo vinaitwa *gangs* na vyenyewe viweze kurekebishwa ili viendane na wakati na wafanyakazi wafanye kazi katika mazingira mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndumbaro halafu Mheshimiwa Frank.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kumekuwa na ahadi ya Serikali ya kujenga reli ya *standard gauge* kutoka Mbambabay - Mchuchuma - Songea mpaka Mtwara. Je, ni lini Serikali itajenga reli hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali la Kibunge hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko kwenye mchakato wa kuhakikisha reli ya Kaskazini ya kutoka Tanga mpaka Musoma na reli ya Kusini kuanzia Masasi mpaka Mbambabay inajengwa kwa kiwango cha kisasa na mpaka sasa hivi ninavyoongea tayari Serikali ilikwishamaliza usanifu wa kina pamoja na upembuzi yakinifu na sasa hivi tuko kwenye hatua za kutafuta mshauri muelekezi wa masuala ya kifedha kwa ajili ya kumpata mwekezaji *under PPP* tukayeshirikiana na Serikali kujenga reli hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA* ni reli ambayo ingeweza kusaidia sana kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam na kupeleka nchi za Congo, Zambia na Zimbabwe na kuepusha uharibufu mkubwa wa barabara ambao umekuwa ukitokea kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma. Tumeshangaa kwamba mizigo mingi wanatumia malori kusafirisha badala ya reli ya *TAZARA*. Je, kuna changamoto gani ambazo Serikali imezigundua kutokana na wafanyabiashara wengi kutokutumia reli hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, reli yetu ya *TAZARA* imekuwa ikifanyakazi kwa muda mrefu sana na imekuwa ikihudumia mizigo pamoja na abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Kapirimposhi nchini Zambia na kusema kweli Shirika letu hilo la *TAZARA* limekuwa likifanyakazi nzuri sana katika huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi karibuni kumejitokeza baadhi ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu ambao walikuwa wanaishauri vibaya Serikali kitendo kilichosababisha sasa tuanze kukosa mizigo kutoka kwa wateja wetu ambao ni muhimu sana ikiwemo kile kiwanda cha kutengeneza saruji ambacho kiko Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi karibuni nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imekwishalifanyia kazi na kuna timu ya wataalam inafuatilia kuhakikisha wateja wetu wote ambao walipotea wanarudishwa. Na sasa hivi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mwakajoka kwamba wateja wale wakubwa tumekwishaanza kuwarudisha na *TAZARA* sasa inafanyakazi nzuri sana. Tuna uhakika ndani ya mwaka mmoja huu wateja wote watakuwa wamesharudi kwa sababu hakuna njia nyepesi na nzuri na salama ya kusafirisha mizigo na abiria kama reli zetu kupitia *TAZARA* na *TRC.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza.

Na. 34

**Ujenzi wa Barabara ya Kanazi - Kyaka**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Kanazi - Kyaka kwa lami na kuimarisha Daraja la Kalebe linalopitisha magari

yenye mizigo tani kumi ili iweze kupitisha mizigo hadi tani 40?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kanazi hadi Kyaka yenye kilometa 55.86 ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Kietama - Kanazi hadi Kyaka yenye urefu wa kilometa 60.65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kukamilisha utekelezaji wa sera yake ya kuunganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani kwa barabara za lami. Baada ya hapo ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara nyingine za mikoa ikiwemo ya Kanazi hadi Kyaka utafuata kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo Wizara ya Ujenzi na uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imeendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hiyo ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka ambapo mwaka 2018/2019 jumla ya shilingi milioni 411.688 zimetengwa kwa ajili ya barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu uhuru barabara hii ni ya vumbi, lakini pia wananchi hawa ni wakulima wakubwa wa kahawa ambao wamekuwa wakichangia katika uchumi katika nchi yetu, lakini pia inashangaza ni namna gani Serikali inawaza zaidi nchi jirani kuliko watu wake ambao wanaendelea kupita katika barabara mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize Serikali kwa sababu miaka ya uhuru ni zaidi ya miaka 50 wananchi wa eneo hili wasubiri sasa miaka mingapi ili barabara hii iweze kutengenezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili nimeuliza swali langu kuhusu daraja la Kalebe lakini Serikali imekwepa kabisa kugusia daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili linasaidia sana wanafanyabiashara na linabeba mizigo ya tani na linapitisha mizigo ya tani 10 badala ya 40 na kuna biashara kubwa ya mbao ambayo wananchi wanahangaika kupitia kutoka Bukoba Vijijini kwenda Kyaka na baadae kurudi Bukoba Mjini na hatimaye sasa kwenda Mwanza, kwa hiyo wanachukua muda mrefu.

Je, kwa sababu mmenionyesha dhamira ya kutokuweza kujenga barabara hii na ndio maana mmepuuza Daraja la Kalebe, sasa naomba nimuulize Waziri daraja hili sasa lina muda upi wa maisha kwa maana ya *life span* linaweza kudumu kwa muda gani ili kabla ya kufanyiwa matengenezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeeleza vipaumbele vya Serikali ambavyo nina hakika hata Mheshimiwa Mbunge naye anakubaliana navyo. Tumejipanga kuunganisha mikoa pamoja na nchi jirani, kisha baada ya hapo tutaenda kwenye barabara za mikoa

kuunganisha sehemu mbalimbali na barabara yake hiyo ya Kyaka ikiwemo. Hatuna nia ya kuipuuza barabara hiyo na ndio maana kupitia bajeti ya mwaka huu ambayo bahati nzuri kabisa mwenzangu yule hakuiunga mkono tumetenga shilingi milioni 411 kwa ajili ya ukarabati ili njia hiyo iendelee kupitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la Daraja la Kalebe ninaomba tuwasiliane naye twende tukaangalie *status* kwa sababu siwezi kumpa majibu ambayo ni nusu nusu ambayo sina uhakika nayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Qambalo

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa, barabara ya Rasimkumbi mpaka Kilindoni kilometa 55 katika kisiwa cha Mafia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne na imo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Lakini mpaka sasa hata usanifu haujaanza.

Swali, je, ni lini Mheshimiwa Waziri barabara hii usanifu utaanza na hatimaye kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Dau, Mbunge wa Mafia kwamba barabara ya Rasimkumbi hadi Kilindoni upembuzi yakinifu tayari umekwishaanza, tukishapata taarifa ya upembuzi yakinifu tutakwenda kufanya usanifu wa kina kwa ajili sasa ya kutafuta pesa kwa ajili ya kujenga eneo hilo. Kwa hiyo, tunaomba avute subira kazi zinaendelea tumekwisha jipanga kwa ajili ya kutekeleza.

**MWENYEKITI:** Na jana mmesikia barabara ya Ilala Mheshimiwa Waziri eeh. Haya Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni zaidi ya miaka miwili na nusu imepita tangu upembuzi yakinifu wa barabara ya Karatu- Mbulu- Haydom ufanyike. Je, ni lini sasa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafurahi kwamba Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba upembuzi yakinifu ulikwishafanyika na usanifu wa kina umekwishafanyika. Kwa hiyo, hatua zinazofuata Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tunatafuta pesa kwa ajili ya kulijenga eneo hilo kwa awamu, na hivi karibuni zitakapopatikana utaona wakandarasi wanaingia pale barabarani kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kawambwa

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia swali la nyongeza.

Je,ni lini Serikali itaendeleza ujenzi wa barabara ya Ludewa- Kilosa - Mikumi kwa kiwango cha lami? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabra aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge tayari ilikwishafanyiwa upembuzi yakinifu na ikafanyiwa usanifu wa kina na hivi karibuni tumekwishapata fedha ambayo itaanza kutekeleza mradi huo awamu kwa awamu. Kwa hiyo, tunamuomba Mheshimiwa Mbunge na

ninamshukuru sana kwa kufuatilia sana barabara za Mkoa wa Morogoro ambazo zinaunganisha avute subira ataona wakandarasi wakiwa eneo la kazi kwa ajili kutekeleza barabara hiyo muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa.

**MHE.DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara ya Bagamoyo hadi Mlandizi ni barabara wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami na wananchi wake kuweza kulipwa fidia zao?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, ajiandae Profesa Jay halafu Mheshimiwa Allan Kiula.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imekwishafanya upembuzi yakinifu wa barabara aliyoitaja kutoka Bagamoyo mpaka Mlandizi, na sasa hivi hatua za usanifu wa kina zinaendelea ili kuhakikisha barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami. Lakini mpaka sasa hivi kuna pesa ambayo imetengwa kwa ajili ya kui-*mantain* barabara hiyo iweze kupitika mwaka mzima. Kwa hiyo, usanifu wa kina utakapokamilika barabara hiyo itaanza kutafutiwa pesa kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Profesa Jay, ajiandae Mheshimiwa Allan

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.Nilishauliza mara kadhaa kuhusu barabara hii ya Dumila- Kilosa – Mikumi na Serikali ilikuwa ikitoa majibu haya haya kuhusu upembuzi yakinifu. Barabara hii ni muhimu

sana na hata mwaka jana tulitengea bajeti kuhusu ujenzi wa kipande hiki cha kilometa 21 kutoka Ludewa kwenda Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nipate majibu ya Serikali, je, ni lini hasa wananchi wanataka kujua ni lini hasa kazi ya ujenzi wa barabara ya kipande hicho cha kilometa 21 Ludewa –Kilosa utakamilika na *then* tutaanza lini ujenzi wa kutoka pale Kilosa kuelekea Mikumi ili wananchi wa Mikumi waweze kufaidi matunda ya Serikali yao?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akisikia mara kwa mara kwamba upembuzi yakinifu tayari, usanifu wa kina tayari. Nimtaarifa tu kwamba hatua hizo mbili zilishafanyika, hatua inayofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Fedha ilikwisha tengwa na hivi karibuni tunaamini katika bajeti ya mwaka huu kipande hicho cha barabara kitaweza kujengwa ili tuwaunganishe watu wa Morogoro na Ludewa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Allan.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Barabara ya kutoka Iguguno mpaka Bukundi ambayo ni Mkoa wa Simiyu inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu, na tunaona sasa daraja la Sibiti linaendelea vizuri kwa ujenzi wake. Ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza kwa jitihada zake mbalimbali anazozifanya katika kuhakikisha kwamba barabara za Jimboni kwake zinapitika muda wote. Na kwa

kweli hata wananchi ambao anawawakilisha wanakiri hilo kwa sababu nilipotembelea kule mara ya mwisho waliniambia jitihada zake anazozifanya na nikawaeleza wananchi wa pale jinsi ambavyo anafika ofisini mara kwa mara kuhakikisha kwamba barabara zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru vilevile kwa jinsi alivyotambua jitihada za Serikali za kuhakikisha lile daraja sasa limekwisha kuwa tayari na linapitika. Lakini wale wakandarasi waliotengeneza lile daraja bado wapo eneo la *site* na ni hao ambao tutawatumia kuhakikisha hicho kipande alichokitaja Mheshimiwa Mbunge kinatengenezwa na kipitike kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante, waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

Na. 35

**Hatima ya Amana za Wateja wa Benki ya FBME**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* inalo jukumu la kuzisimamia benki nyingine hapa nchini pamoja na kulinda haki za wateja wa benki za biashara. Kwa zaidi ya miaka miwili sasa Benki ya FBME imefungwa kwa sababu ya ukiukwaji wa sheria za kifedha na mpaka sasa jambo hilo halijapatiwa ufumbuzi.

(a) Je, ni sababu gani inayofanya benki hiyo isiwalipe wateja wake haki zao au amana zao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa *BOT* imeshindwa kutimiza wajibu wake wa kuzisimamia benki nyingine na kuwafanya wananchi kukosa imani na mifumo ya kibenki inayorudisha nyuma utaratibu wa kuhifadhi fedha?

(c) Je, Serikali haioni kuwa tunakosa mapato ambayo yangetusaidia kwa ajili ya maendeleo ya nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 11(3)(i), 41(a), 58(2) na 61(1) vya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 Benki Kuu ya Tanzania ilisimamisha shughuli zote za Benki ya FBME na kufuta leseni ya biashara, kuiweka chini ya ufilisi na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana kama mfilisi tarehe 8 Mei, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua hiyo, jukumu la kuwalipa wateja wa Benki ya FBME haki au Amana zao kisheria lipo mikononi mwa Bodi ya Bima ya Amana na siyo Benki ya FBME. Malipo ya fidia au amana kwa wateja yamechukua muda mrefu kwa sababu ya taratibu za kisheria zinazotakiwa kuzingatiwa katika zoezi zima la ufilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, zoezi la kulipa fidia kwa wateja waliokuwa na amana katika Benki ya FBME kwa mujibu wa sheria lilianza mwezi Novemba, 2017 na bado linaendelea. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Julai, 2018 asilimia 60 ya wateja wa benki hiyo walikuwa wamelipwa fidia ya amana na Bodi ya Bima ya Amana.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya msingi ya Benki Kuu ni kusimamia utendaji wa kila siku wa taasisi za kifedha hususan benki. Katika kutekeleza jukumu hili, Benki Kuu kuchukua hatua kuinusuru benki husika ikiwemo kusimamia uendeshaji wa shughuli za benki au kuifutia leseni mara tu inapobaini viashiria vya kufilisika au upungufu mkubwa wa ukwasi kinyume na matakwa ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na Kanuni

zake. Lengo la kufanya hivyo ni kulinda walaji, amana za wateja na kujenga imani ya wananchi kuhusu mifumo ya benki na utaratibu wa kuhifadhi fedha kwenye mabenki.

Pili, Benki Kuu husimamia taratibu zote za ufilisi kwa taasisi itakayofutiwa leseni na kuhakikisha kuwa wateja wanapata fidia kwa mujibu wa sheria. Kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo, majukumu haya mawili yanaendelea kutekelezwa na kusimamiwa vizuri na Benki Kuu. Hivyo basi, siyo kweli kwamba Benki Kuu imeshindwa kuzisimamia taasisi za fedha na benki na hivyo kuwafanya wananchi kukosa imani na mifumo ya kifedha nchini

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kuwa Taifa linakosa mapato ambayo yangesaidia kuleta maendeleo, ni lazima kuzingatia matakwa ya kisheria, kanuni na taratibu zilizopo ili zoezi hili liweze kufanyika kwa ufanisi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, zoezi la ufilisi linafanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za ufilisi wa kampuni. Napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Mfilisi wa Benki kwa kushirikiana na Benki Kuu anafanya juhudi za kukusanya madeni pamoja na fedha za benki zilizopo kwenye benki nyingine nje ya nchi ili kulipa amana za wateja kwa kadri itakavyowezekana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimkumbushe tu kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa vile alikuwa ni mwalimu wangu *kullu-kum rai, wakullu-kum mas-ul alayhi.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliokuwa wafanyakazi wa benki ambayo waliondolewa kazini na wasimamizi wa *Deposit Insurance Board (DIB)* ndio wakasimamia ufilisi wa benki hiyo. Hawajalipa wafanyakazi hao mpaka sasa hivi na ukizingatia ni wapiga kura wetu, ni wananchi wetu kwa muda mrefu sasa hivi. Je, haioni sheria hiyo aliyoitaja kuwa imepitwa na wakati na inawakandamiza wananchi na lini ataleta sheria hiyo? *That is (a).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili katika majibu yake alisema kukusanya madeni pamoja na fedha za benki zilizopo kwenye benki nyingine nje ya nchi na kulipa amana za benki, nataka nimwambie tu *FBME correspondence bank* ni *Dutch Bank* hebu tuambie kiasi gani ambazo ziko huko na lini zitaletwa ili wananchi hao na Serikali kukosa mapato. Na hivi juzi tumeshuhudia makontena kupigwa mnada wananchi wanataka kununua makontena hayo ili wapate biashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza ni swali la wafanyakazi wa iliyokuwa Benki ya FBME. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, taratibu za wafanyakazi zinashughulikiwa na sheria za kazi za Taifa letu. Kwa hiyo, wafanyakazi wale walipoajiriwa na benki hii walisaini mikataba na hivyo sheria za kazi za Taifa letu zinaendelea kusimamia haki ya wafanyakazi wote waliokuwa wa benki hii ya FBME.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili napenda kumwambia Mheshimiwa Jaku Hashim kwamba avute subira tunaendelea kufuatilia kama anavyofahamu yeye kwamba benki hii ilikuwa ni benki ambayo asilimia 10 ya uendeshaji wake ulikuwa ndani ya Taifa letu na asilimia 90 ulikuwa nchini Cyprus. Kama Wizara na Benki Kuu tunaendelea kulifuatilia jambo hili kwa ukaribu na tunawahakikishia wateja wetu watapata fedha zao kwa muda muafaka.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

Na. 36

## Hitaji la Mabanio Katika Mto Katuma

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Novemba, 2016 Serikali ilivunja mabanio (vizibo) vya maji katika Mto Katuma, Mto Mpanda na Mto Mafunsi ambayo yalikuwa yanasaidia wakulima wa zao la mpunga na mengineyo katika Mkoa wa Katavi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabanio (vizibo)ili matumizi ya maji yawe haki kwa kila kiumbe kama sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji; naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 kifungu namba 43 kinamtaka mtu yeyote anayetaka kuchepusha au kuchukua maji kutoka chanzo chochote cha maji ikiwemo mito, maziwa, mabwawa au maji chini ya ardhi lazima awe na kibali na awe kibali cha kutumia maji kutoka Bodi ya Maji ya Bonde husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Novemba, 2016 Serikali ilivunja miundombinu ya umwagiliaji (mabanio) iliyopo katika Mito ya Katuma, Mpanda na Mifunsi kutokana na miundombinu hiyo kujengwa bila kuwa na vibali vya kutumia maji kama sheria inavyoelekeza, hivyo kusababisha Mbuga ya Katavi na Vijiji ambavyo viko chini kukosa maji. Mwezi Agosti, 2017 Wizara kupitia Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mpanda iliainisha maeneo nane yanayofaa kujengwa miundombinu ya umwagiliaji katika Mito ya Katuma, Mpanda na Mafunsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.750 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo katika Mito ya Katuma, Mpanda na Mafunsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE.RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mito inapeleka mpaka Mbuga ya Katavi lakini kwa mujibu wa sheria watu wote wana haki. Sasa niombe ni lini sasa Serikali itakamilisha kandarasi hiyo upembuzi yakinifu ili katika bajeti ya mwaka 2019/2020 tuweze kutengewa fedha kwa ajili ya skimu ya umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna mradi wa umwagiliaji uliopo kwenye kata ya Ugala ambapo una miaka mingi haujakamilika na mifereji bado na unasimamia na Mamlaka ya Bonde makao makuu yaliyoko Mbeya. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha ili kukamilisha mradi huu ili uweze kutumika na wananchi katika uzalishaji na kuinua maeneo yao ya kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri na namna anavyofuatilia changamoto za wananchi wake. Kubwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji kutokana na changamoto hiyo katika umwagiliaji, tumeona haja sasa ya kufanya upembuzi wa haraka. Kubwa ambalo nataka nimhakikishie, tutafanya usimamizi wa haraka ili mwisho wa siku hili jambo liweze kukamilika na ujenzi ule uweze ujengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la ukamilishaji wa mradi aliouelezea, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara yetu ya Maji tumeainisha miradi ambayo haijakamilika. Tumeona tumekuwa na miradi zaidi ya 1,967 ambayo haijakamilika. Kwa hiyo, wajibu wetu ni kuhakikisha tunaikamilisha ili mwisho

wa siku iwe na mchango mkubwa sana katika uchumi wetu wa kati. Tunajua kabisa umwagiliaji ni kilimo cha mbadala ambacho kina mchango mkubwa kabisa katika suala zima la uchumi kwa maana ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalisimamia hili jambo mradi wao ukamilike ili uweze kuwa na tija kwa wananchi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi, halafu Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi wa Umwagiliaji wa Mwamkulu ni takribani miaka nane sasa haujakamilika na wananchi wa eneo hilo walivunjiwa vizibo. Napenda kuiuliza Serikali, ni lini itapeleka fedha ili kuhakikisha mradi huo umekamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri. Nimhakikishie kwamba hili jambo ni la haraka. Kwa hiyo, sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga katika kuhakikisha tunalikamilisha hili jambo ili wananchi wake waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge pia baada ya saa saba mchana tunaweza tukakutana tujadiliane kwa pamoja ili tuone ni namna gani tunaweza tukalifanya hili jambo ili liweze kukamilka kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe ni Mji unaokuwa kwa kasi sana na upo katika Miji 17 ambayo imeahidiwa kutengenezewa miradi mikubwa ya maji na Mji wa Njombe unategemea kupata maji kutoka Mto wa Gafilo.

Je, ni lini huu mradi sasa utaanza ili kusudi wananchi wa Njombe waweze kupata maji safi na salama?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji na tunatambua kabisa katika Mkoa wa Njombe ni moja ya Mikoa ambayo ina changamoto kubwa sana katika suala zima la maji. Wizara yetu ina miradi zaidi ya 17 kwa maana ya mkopo nafuu katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo lolote kubwa ambalo lina mafanikio makubwa, lazima linakuwa na taratibu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuko katika taratibu za manunuzi. Pindi manunuzi yatakapokuwa yamekamilika, tutampata Mkandarasi katika kuhakikisha mradi ule unakamilika kwa wakati kwa wananchi wake wa Njombe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Nagu, halafu ajiandae Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa kuendesha vizuri Bunge letu na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang ni moja ya Wilaya ambazo mvua hazina uhakika na ninaishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa Endagau wa umwagiliaji. Hata hivyo, mradi huo ulikuwa na mushkeli. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kama wametoa fedha za kutosha kusahihisha yale mambo ya

kitaaluma ambayo hayakwenda vizuri na umwagiliaji hauendi vizuri ili wananchi wa Hanang waweze kuwa na uhakika wa kupata chakula kutokana na umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ajiandae Mheshimiwa Kaboyoka.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu imekuwa inafanya jitihada kubwa sana ya kutoa fedha katika kuhakikisha inakamilisha miradi mbalimbali. Itakuwa ni jambo la aibu na fedheha kwamba tunapeleka fedha halafu hazifanyi kazi kama ilivyotarajiwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge tutafika hapo katika Jimbo lake ili kuweza kuhakikisha kama fedha zimepelekwa, nao kwa nini wasizitumie kama ilivyotarajiwa? Kama kuna ubadhirifu wowote, tutaweza kuchukua hatua kwa wale wahusika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Aaah!

**MWENYEKITI:** *Sorry,* Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunikumbuka ingawa ulitaka tena unifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Waziri wa Maji kwamba Jimbo la Same Mashariki lina mito mingi ambayo inatumika kwa umwagiliaji wa mpunga na tangawizi, lakini maji hayo yanapungua kila kuitwapo leo.

Je, Wizara ina mkakati gani wa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili wapate fedha ya kusaidia kutunza vyanzo vya maji ya mito hii mikubwa iliyoko katika Jimbo la Same Mashariki? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa na vyanzo vingi sana katika nchi yetu, lakini kiukweli ukipita maeneo mbalimbali kuna baadhi ya vyanzo vimekauka, vingine vimefikia hatua hata kupotea, ni kwa sababu tu moja, ni mabadiliko ya tabia nchi, lakini pili, shughuli za kibinadamu, watu kulima karibu na vyanzo vya maji, wengine kufanya suala zima la ufugaji na wakati mwingine hata shughuli za uchimbaji madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maji tuna mabonde, kazi yao kubwa sana ni kusimamia rasilimali za maji ili ziweze kuwa endelevu. Kingine tunapokea ushauri kuweza kushirikiana na wenzetu hawa wa mazingira katika kuhakikisha tunavilinda na kuvitunza vyanzo vya maji viwe na faida ya sasa na vizazi vijavyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kabati.

Na. 37

**Mradi wa Umwagiliaji Iringa Mjini**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji wa *Mkoga Irrigation Scheme* uliopo katika Manispaa ya Iringa Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutekeleza ujenzi wa *scheme* mbalimbali hapa nchini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kupitia mfuko wa *Food Aid Counter Party* ilitumia kiasi cha shilingi milioni 270 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mashambani na ujenzi wa mfereji mkuu katika *scheme* ya umwagiliaji ya Mkoga yaani *Mkoga Irrigation Scheme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu wa *scheme* hiyo haujakamilika na bado unahitaji kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya umwagiliaji mashambani. Hivyo Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeingiza *scheme* ya umwagiliaji ya Mkoga kwenye awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango kabambe wa Taifa wa umwagiliaji utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi mwaka 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza, lakini kabla sijauliza nilikuwa naomba nisahihishe jina langu, naitwa Ritta Enespher Kabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na mpango wao kabambe wa umwagiliaji, naomba nimwulize maswali mawili.

Kwa kuwa mradi huu wa Mkoga umekuwa ni mradi wa muda mrefu sana toka umeanzishwa katika Manispaa yetu. Tulikuwa tunategemea kama mradi huu ungekamilika, ungeweza kunufaisha zaidi ya wananchi 400 wakiwemo akina mama na vijana kuweza kujiajiri katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie katika mwaka wa fedha 2019/2020 kama Serikali itaweza kutoa pesa ili kuweza kuukamilisha huu mradi ambao umekuwa wa muda mrefu sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nilikuwa nataka kuuliza kwamba kwa kuwa katika Manispaa yetu hii ya Iringa bado tunao mradi mwingine wa *Kitwiri Irrigation* mradi ambao pia toka umeanzishwa haujawahi kupatiwa fedha, je, ni lini utapatiwa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namwomba Mheshimiwa Waziri kama yuko tayari kuja sasa katika mkoa wetu wa Iringa ili aitembelee hii miradi yote miwili na vilevile atembelee hata miradi mingine ya mkoa wetu wa Iringa ili iweze kukamilika na iweze kunufaisha wananchi wa mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, mama yangu Mheshimiwa Ritta Kabati, ni mmoja ya wamama shupavu sana katika kuhakikisha wanatetea matatizo ya wananchi wao katika Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu, tumekuwa na miradi mingi sana katika umwagiliaji zaidi ya 2000 lakini ni miradi 960 tu ndiyo iliyoendelezwa, zaidi ya miradi 1,967 haijaendelezwa. Sisi kama Wizara ya Maji, tukitambua kabisa umwagiliaji ndiyo kilimo mbadala ambao kinaweza kuchangia uchumi wa nchi yetu, tumeona haja sasa ya kuunda Tume ambayo itapitia mpango kabambe wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili tuwe na miradi michache ambayo itakuwa na tija kubwa sana katika nchi yetu kwa sababu tumekuwa na miradi mingine haina hata chanzo cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la umwagiliaji, maana yake ni kilimo cha mbadala. Tunajua kabisa nchi yetu wakulima wengi wanalima kwa kutegemea kudra za Mwenyezi Mungu mpaka mvua inyeshe. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie, katika mpango huu kabambe tutakaoupitia katika mradi huu wa Mkoga, tutaupa kipaumbele katika kuhakikisha tunaukamilisha ili wananchi

wake wa Iringa waweze kunufaika na kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu mimi kwenda Iringa, nataka nimwambie mwenda kwao haogopi kiza. Nitakwenda Iringa katika kuhakikisha naenda kuzungumza na wananchi wa Iringa ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Balozi Mwamoto na ajiandae Mheshimiwa Nswanzugwako.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Kata Ruaha Mbuyuni iko Kilolo - Iringa, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kupita pale na kutoa ahadi, lakini baadaye Waziri husika alifika mwaka 2017 tarehe 28 Desemba akatoa ahadi kwamba Halmashauri ifanye *designing* na ipeleke mradi ule Wizarani ili yeye atoe kibali cha kutangaza. Sasa hivi imeshachukua muda mrefu na wananchi wanaendelea kusubiri.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri naye anasemaje ili wananchi wa Ruaha Mbuyuni waweze kupata uhakika kwamba sasa watapata maji safi na salama ili kipindupindu ambacho kimekuwa kikiwaua kwa muda mrefu kiache kuwaua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Wajiandae Mheshimiwa Nswanzugwako, Mheshimiwa Monko na Mheshimiwa Chikambo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua maji ni huduma muhimu sana kwa wananchi na kwa kuwa hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi tunatambua kabisa ahadi ni deni. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi hiyo tutaietekeleza ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi salama na yenye kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nswanzugwako.

**MHE. DANIEL N. NSWAZUNGWAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nina swali dogo la nyongeza kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Scheme* ya Umwagiliaji ya Msambala katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu ni *scheme* ambayo imetelekezwa, ina chanzo cha uhakika cha maji, lakini haipati fedha. Napenda kujua toka kwenye Wizara, ni kwa nini mradi huu muhimu umetelekezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Nia yetu sisi kama Serikali hatuna haja ya kutelekeza miradi, ila tumeona haja sasa ya kuunda Tume kubaini miradi ambayo itakuwa na tija kwa nchi yetu katika kuhakikisha tunaipelekea fedha ili iweze kuwa na tija kwa wananchi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monko, halafu Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Suke lililopo katika Kijiji cha Msange lilifanyiwa upembuzi tangu mwaka 2010 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwenye Kata ya Msange, Makhojoa, Mwasawila na nyingine. Bwawa hili lilihitaji shilingi 1,300,000,000 na tangu mwaka 2010 hatujatengewa fedha mpaka sasa.

Je, ni lini tutapata fedha hizo kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa bwawa hilo ili wananchi waache kutegemea kilimo cha mvua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Wajiandae Mheshimiwa Chikambo na Mheshimiwa Yosepher.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwona mtu mzima analia, ujue kuna jambo. Naona Mheshimiwa Mbunge amelia sana kuhusu wananchi wake. Nataka niwahakikishie tutaona haja basi katika bajeti ya mwaka 2019/2020 ili tuangalie namna gani tunaweza tukasaidia hili jambo ili wananchi wake waweze kunufaika na mradi huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini iko miradi mingi ya maji ya umwagiliaji katika Mkoa wangu wa Ruvuma ambayo haijakamilika ikiwemo miradi ambayo iko katika Vijiji vya Legeza Mwendo, Misiaje na Kitanda Wilayani Tunduru. Miradi hii ilitakiwa ikamilike kupitia mpango wa *ASDP* Awamu ya Kwanza, lakini mpaka leo haijakamilika kwa ukosefu wa fedha.

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha tunapeleka fedha za kukamilisha miradi hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Chikambo kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini kikubwa kama nilivyoeleza tumekuwa na miradi mingi ambayo haijakamalika, nasi kama Serikali tumeona haja ya haraka ya kuunda Tume.

Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge, subira yavuta heri. Heri itapatikana pindi Tume itakapotuleta majibu ya haraka nasi tutaweza tukakamilisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yosepher, halafu Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Misozwe, Jimbo la Muheza ambao umekamilika zaidi ya miaka kumi, lakini mradi ule mpaka sasa hivi haujaanza kwa sababu wananchi wa eneo lile ambalo lina mradi hawajalipwa fidia.

Je, ni lini watalipwa fidia ili waweze kupisha mradi uanze?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Mheshimiwa Ngombale na Mheshimiwa Gulamali wajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa na nia ya utekeleza wa miradi mikubwa kwa ajili ya manufaa kwa wananchi, lakini zipo athari kwenye utekelezaji wa miradi kupita maeneo ya watu. Nataka niwahakikishie wananchi hawa, sisi kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji tutahakikisha kwamba wale wananchi wanaostahili kulipwa wanalipwa fidia. Ila tutamlipa mwananchi anayestahili kulipwa na yule asiyestahili hatalipwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTUS E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iliingia mkataba na wenzetu wa *DDCA* kwa ajili ya kuchimba visima virefu toka mwaka 2017, lakini mpaka sasa mradi huu haujatekelezwa. Ni lini *DDCA* watatekeleza mradi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lini? Lakini unakwenda vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, lakini kubwa nampongeza Mheshimiwa Mbunge, Wizara yetu ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji. Sisi Wizara ya Maji siyo Wizara ya ukame nawaagiza ndugu zangu wa *DCAA* kuhakikisha miradi hiyo wanachimba kwa haraka

ili wananchi wako wapate maji safi salama na yenye kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kujua, pale katika *scheme* yetu ya umwagiliaji ya Choma Chankola tuna *scheme* ya umwagiliaji na Mheshimiwa Waziri alishawahi kuja kuona lile eneo na akaahidi tupeleke andiko kwa ajili ya uchimbaji wa bwawa kubwa pale. Tayari andiko limeshapelekwa katika Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Sasa ni lini fedha zitaweza kutolewa kwa ajili ya uchimbwaji wa bwawa hilo kwa sababu tayari ishapita miaka mitatu?Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu kwa kifupi. Mheshimiwa Haonga na Mheshimiwa Yahaya wajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kaka yangu, Mheshimiwa Gulamali kwa namna anavyowatetea wananchi wake, lakini kubwa nataka nimhakikishie kwamba nami naomba nipitie hilo andiko kwa haraka ili mwisho wa siku tupate kushauriana na Mheshimwia Waziri wangu mpya, Mheshimiwa Mbarawa katika kuhakikisha hili jambo tunalikamilisha kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga halafu Mheshimiwa Yahaya.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, mashamba mengi ya kahawa Wilayani Mbozi katika Kata za Magamba, Nambinzo, Iyula na Igamba yameendelea kukauka. Ni lini Serikali itachimba mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji wa kahawa katika maeneo haya ambapo

kahawa sasa inaendelea kukauka na hali imekuwa ni mbaya sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza sisi nchi yetu tunataka kwenda kwenye kilimo lakini kimekuwa na changamoto nyingi sana. Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji tumeona haja sasa ya kuingia katika kilimo cha umwagiliaji. Kama nilivyoeleza, tuna Tume yetu ambayo inapitia maeneo mbalimbali kubainisha yale maeneo ambayo tunaweza tukahakikisha kwamba tunajenga hayo mabwawa. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Haonga, sisi kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi hao katika kuhakikisha tunatengeneza mabwawa hayo ili yaweze kuwa na faida kwa wananchi wao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, Serikali imedhamiria kufanya kazi nzuri sana hasa katika Jimbo langu, imejenga bwawa na inajenga *scheme* ya umwagiliaji katika Bwawa la Ikagata, lakini kuna fedha kiasi cha shilingi milioni 180 na zaidi za *scheme* ya umwagiliaji ziliazimwa kwa ajili ya kuziba bwawa hili ambalo lilikuwa linavuja.

Je, ni lini Serikali itarudisha fedha katika mradi ule ili Mkandarasi aweze kulipwa, amalizie kazi hii ambayo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano na Wizara yenu iko na nia njema kwa wananchi wa Jimbo langu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk jiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa ufupi tu nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge saa saba mchana

tuweze kukutana ili niweze kupata maelezo vizuri zaidi ili nami niweze kuhakikisha kwamba nalisimamia hili jambo liweze kukamilika kwa wakati. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nashukuru kwa mradi wa vijiji kumi katika kila Halmashauri, mradi wetu wa maji ule unakwenda vizuri.

Je, Serikali ina mpango gani katika vile vijiji ambavyo havitapitiwa na ule mradi wa vijiji kumi wa kuwachimbia visima virefu ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nimjibu Mheshimiwa Mbunge wa Mkoa wangu wa Tanga, kaka yangu Mheshimiwa Mussa kwamba Wizara yetu ya maji kama nilivyoeleza, jukumu letu ni katika kuhakikisha tunawapatia wananchi maji mijini na vijijini na lengo la Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ni kufikia asilimia 85 katika kuhakikisha vijijini wanapata maji. Sisi kama Wizara ya Maji tuna taasisi mbalimbali kwa maana ya *DDCA* katika kuhakikisha kwamba tunachimba visima hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mhandisi wa Maji katika Jimbo lake alete andiko, nasi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha tunawasaida wananchi wa Tanga. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma.

Na. 38

**Fidia kwa Wanachi wa Mtwara Mjini**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haisemi ukweli Bungeni juu ya fidia kwa wananchi wa Mtwara Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mkubwa wa fidia uliopo sasa katika Manispaa ya Mtwara Mikindani unahusu eneo la Mjimwema na Tangira unaotokana na upimaji wa viwanja 10,000 uliotarajiwa kufanywa kwa njia ya ubia baina ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, pamoja na Taasisi ya *UTT-PID* mwaka 2003. Upimaji huu haukufanyika kama ilivyopangwa kutokana na amri ya kusitishwa kwa miradi yote ya upimaji wa viwanja ambavyo Halmashauri mbalimbali zilikuwa zikishirikiana na *UTT-PID* iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na katazo hilo, Manispaa ya Mtwara Mikindani iliendelea kuomba kibali cha kuendelea na mradi huo, kwa kuwa shughuli mbalimbali tayari zilikuwa zimeshafanyika zikiwemo uthamini kwa ajili ya fidia. Baada ya ufuatiliaji, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa kibali cha kuendelea na mradi huo kwa barua yenye Kumb. Na. GB.2013/234/01/117 ya tarehe 2/09/2016.

Hata hivyo mwishoni wa mwaka 2017 Taasisi ya *UTT-PID* ilikiri kutoweza kuendelea na mradi huo kutokana na ukosefu wa fedha uliosababishwa na taratibu za utekelezaji wa mradi huo kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Januari, 2018 Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani liliamua kuendelea na mradi huo kwa kuwapimia wananchi maeneo yao na kisha kuwapa viwanja kulingana na ukubwa wa maeneo yao na hatimaye kuwamilikisha kisheria badala ya kusubiri fidia ambayo kimsingi haipo. Jumla ya shilingi milioni 170 zilitengwa katika bajeti ya Halmashauri kwa ajili ya kugharamia zoezi la upimaji na ufunguzi wa barabara za msingi katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa eneo la Tangira katika Kata ya Mitengo waliridhia kuendelea na utaratibu wa kupimiwa viwaja katika mashamba yao. Mpaka sasa jumla ya viwanja 1,212 vimepimwa. Aidha, jumla ya viwanja 2,800 vinatarajiwa kupimwa katika eneo la Mjimwema Kata ya Magengeni. Kwa maeneo mengine upimaji wa viwanja utaendelea baada ya kukamilika kwa majadiliano baina ya Serikali na wananchi ambao ni wamiliki wa asili wa mashamba husika.

**MWENYEKITI:** Naam, Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza swali langu halijajibiwa. Niliuliza kwa nini Serikali haisemi ukweli ndani ya Bunge? Kwa sababu hapa nina *Hansard* mbili Serikali ikiahidi kulipa fidia wananchi hawa, lakini pia kuna maelezo ambayo siyo sahihi sana kwenye maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Serikali hii ya Awamu ya Tano inafanya mambo makubwa sana, imeweza kununua ndege, imeweza kuwa na mkakati wa kujenga *standard gauge*, lakini pia imeweza kuweka mkakati wa kujenga *Stiegler's Gorge,* inashindwaje kulipa fidia ya shilingi bilioni nane kwa wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini maeneo ya Mjimwema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba kujua, katika kuilazimisha Halmashauri sasa kuwaeleza wananchi

waweze kupimiwa viwanja, wapo wananchi waliokubali na wengine hawajakubali. Je, kwa kuwa hili suala la Taasisi ya *UTT-PID* ipo ya chini ya Serikali Kuu, Serikali iko tayari hivi sasa kuja Mtwara Mjini na kuweza kutoa elimu kwa wananchi hao wa Mjimwema na Tangira ili waweze kukubaliana na maamuzi ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kutokana na swali lake jinsi alivyouliza, majibu ya Serikali ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitaka kujua kwa nini Serikali haisemi ukweli Bungeni juu ya fidia ya wananchi wa Mtwara? Na sisi tumeongelea habari ya fidia aliyoitaka ya *UTT*. Mpaka sasa hivi anavyozungumza *UTT* haidaiwi kulipa fidia yoyote kwa wananchi wale kwa sababu tayari Manispaa imeshachukua mradi ule na zoezi limeshaanza na wananchi wanapimiwa na kuna makubaliano ambayo wameingia kati ya wananchi na Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kule hakuna anayedai fidia, kwa maana hiyo, kwa sababu tayari baada ya *UTT* kujitoa wananchi kupitia Halmashauri yao wameamua kuchukua eneo lile na kuanza kupimiwa na viwanja wanapewa kama sheria inavyosema. Kwa hiyo, Serikali imejibu kulingana na swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili analotaka habari ya kutoa elimu, sisi tuko tayari wakati wowote tunatoa elimu, tuna vipindi mbalimbali na hata wakitaka twende kule tutakwenda kwa sababu ndiyo kazi yetu kuelimisha wananchi ili waweze kuelewa haki zao za msingi na waweze kufanya mambo yao pasipo kubughudhiwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu siyo rafiki tunaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha.

Na. 39

**Ugonjwa wa Lupa**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA** aliuliza:-

Je, nini chanzo cha ugonjwa wa Lupa na ni watu wangapi wameugua na wangapi wamefariki kutokana na ugonjwa huo hapa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Lupa au kwa jina la kigeni unajulikana kama *Systematic Lupus Erythematosis*ni ugonjwa wa kinga za mwili ambao hushambulia viungo vya mwili vikidhania kwamba ni vitu vigeni *(foreign bodies).* Viongo ambavyo hudhurika zaidi ni ngozi, figo, ubongo, chembechembe za damu, moyo, mapafu na viungo vingine vya mwili kama *joints*. Watafiti hadi sasa hawajaweza kubaini chanzo cha ugonjwa huu. Inasadikiwa kwamba mgonjwa mwenye vinasaba vya Lupa hupata ugonjwa huu pale anapokutana na visababishi kwenye mazingira vinavyochochea kuanza kwa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vinavyoweza kuchangia kuanza kwa ugonjwa huu ni miale ya jua, maambukizi ya bakteria, matumizi ya baadhi ya dawa za shinikizo la damu, dawa za kifafa na *antibiotic*. Wagonjwa wenye ugonjwa wa Lupa unaotokana na dawa hupona haraka mara wanapoacha kutumia dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visababishi vingine vinavyoongeza uwezekano wa kupata ugonjwa huu wa Lupa

ni pamoja na jinsia. Ugonjwa huu huwapata zaidi wanawake kuliko wanaume. Katika masuala ya umri, Lupa huwapata zaidi watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 45. Asili, Lupa huwapata zaidi Wamarekani wenye asili ya Kiafrika, Wahispania na Waasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili za ugonjwa huu siyo rahisi kubainika kirahisi. Baadhi ya dalili kuu ni maumivu ya viungo, uchovu wa mara kwa mara, homa, vidonda vya mdomoni na vipele vinavyofanana na mabawa ya kipepeo kwenye mashavu. Ugonjwa huu hauna tiba, dawa zinazotolewa hulenga kupunguza athari za ugonjwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili takribani wagonjwa wawili hugundulika na ugonjwa wa Lupa kwa mwaka na hufuatiliwa katika Kliniki ya Ngozi. Mpaka hivi sasa kuna wagonjwa takribani 10 wanaofuatiliwa katika hospital hii. Katika mwaka 2017/2018 kumeripotiwa kifo kimoja kutokana na ugonjwa huu. Kuna uwezekano wa vifo vingi zaidi kutokana na ugonjwa huu, lakini havijaripotiwa kutokana na dalili za ugonjwa huu kutobainika kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nimalizie kwa kusema kuwa ugunduzi wa ugonjwa wa Lupa ni mgumu sana na wakati mwingine mtu hutibiwa kama mgonjwa wa ngozi tu. Ni kutokana na ugumu uliopo wa kugundua na hata mtu kujua kama na ugonjwa wa Lupa, wagonjwa wengi hufika katika Hospitali wakiwa na matatizo mengine kama ya ngozi, viungo na hutibiwa matatizo waliokuja nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara ili kugundua kitu chochote kisichokuwa cha kawaida katika miili ili waweze kupata tiba mapema kabla tatizo halijawa kubwa zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jecha, halafu ujiandae Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kama alivyoeleza kwamba ugonjwa huu hapa kwetu upo, pamoja na kwamba anasema wanaoathirika zaidi ni Marekani, lakini hapa kwetu tayari umeingia na mazingira yake tumeona kwamba wanawake waathirika zaidi lakini na umri ni miaka 15 mpaka 45.

Je, Serikali haioni haja ya kuelimisha juu ya ugonjwa huu kwa sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kama ilivyo katika magonjwa mengine, wajibu wetu Serikali ni kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na magonjwa mbalimbali, vyanzo vyake, dalili zake na matibabu yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuhamasisha jamii kupata uelewa wa kina katika jambo hili, Serikali kupitia Kitengo chake cha Elimu ya Afya kwa Umma, tutaweka utaratibu wa kutoa elimu kwa jamii ili wananchi nao waweze kupata uelewa vizuri wa ugonjwa huu.

Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, siyo ugonjwa ambao unabainika kirahisi, wala chanzo chake kinajulikana kirahisi na wala matitabu yake siyo rahisi kama nilivyogusia katika jibu langu la msingi. Kwa hiyo, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutazingatia katika mpango wetu wa elimu ya afya kwa umma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Magonjwa yako mengi kama alivyosema huu ugonjwa wa Lupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Ebola ni hatari sana. Ugonjwa huu umejitokeza nchini *DRC Congo* (Kivu Kaskazini) na umeshaua zaidi ya watu 77 na watu 116 wamegundulika wana ugonjwa huu na kwa sababu sisi Congo, Kivu Kaskazini inapakana na Rwanda, Burundi na Uganda: Je, Serikali kwa sababu ugonjwa huu ni hatari sana, tunamwomba Mwenyezi Mungu apishie mbali ugonjwa huu usije kwetu nchini; Serikali imejipangaje kukabiliana na ugonjwa huu hatari na mbaya sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali zuri. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Ebola ni ugonjwa hatari na unaambukiza kwa haraka sana na mara nyingi ugonjwa huu hauna tiba na wale wanaopata ugonjwa huu zaidi ya asilimia 50 hawaponi, huishia kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa takwimu ambazo amezitoa Mheshimiwa Mbunge kwamba wenzetu katika nchi ya *DRC* limejitokeza balaa hili la ugonjwa wa Ebola na mpaka sasa hivi zaidi ya watu 76 wamefariki na zaidi ya 100 wameugua ugonjwa huu. Sisi kama Tanzania tumechukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumeimarisha mifumo yetu ya ufuatiliaji wa wagonjwa katika mipaka yetu yote kwa kuhakikisha kwamba watu wote wanaoingia nchini katika maeneo ambayo tunayahisi yanaweza yakawa ugonjwa huu, tumeimarisha mfumo wa ufuatiliaji; tumeweka *thermo scanner,* tumeweka maeneo mahususi kwa wale watakaoingia nchini ambao tunawahisi wana dalili, tunawatenga, tumeweka hizo *isolation center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumetoa elimu ya kutosha katika mikoa yetu ambayo ipo mipakani kwa viongozi wote wa Serikali pamoja na watoa huduma wetu wa afya ili endapo mgonjwa ataingia nchini, waweze kuchukua hatua kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesambaza vifaa vya kujikinga *(personal protection equipment)* katika maeneo yote ambayo yapo pembezoni ili watoa huduma wetu na wale ambao wataingia, watakutana na wale wagonjwa waweze kujikinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeimarisha mifumo yetu ya maabara, endapo tutapata mgonjwa ambaye atahitaji kuchukuliwa sampuli, tumenunua vifaa, tunavyo na maabara tumeziandaa.

Mwisho kabisa, tumeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na gonjwa hili kuu, kwamba endapo mtu atamwona mtu ambaye ametoka katika nchi za jirani ana dalili za homa, ana maumivu ya viungo ama kutoka damu sehemu mbalimbali za mwili, wananchi waweze kutoa taarifa kwa haraka katika mamlaka na kuchukua tahadhari ya kutomshika mtu yule ambaye ana dalili zile ambazo nimezigusia. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli Serikali imetoa elimu kwa wananchi wanaoishi mikoani juu ya maambukizi ya ugonjwa wa Ebola, lakini kituo cha kuhudumia wagonjwa wa Ebola endapo watapatikana kipo pale Temeke. Sasa kwa nini Serikali haioni haja ya kutoa elimu hiyo ya uelewa kwa wananchi wa Temeke pia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana. Kuna swali lingine la Mheshimiwa Mwilima.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kituo cha *Isolation Center* kwa magonjwa haya hatarishi kipo pale Temeke, watoa huduma wetu katika Hospital ya Temeke wameshapewa Elimu hiyo na tutaendelea kutoa elimu kwa

ujumla kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na wananchi wa Temeke kuhusiana na athari za ugonjwa huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwilima**.**

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Jimbo la Kigoma Kusini tunapakana na nchi ya Congo kwenye vijiji 27 na niliona juzi/hivi karibuni wakati Mheshimiwa Waziri anatoa tamko la kupata ugonjwa huu, ukawa unaweza kuingia nchini, tuliona Kigoma kuna mtu mmoja tu ambaye alioneshwa kwenye *tv* kwamba yupo peke yake na kifaa anachotumia ni kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangaliza kwa mazingira ya Mkoa wa Kigoma, Jimbo hili la Kigoma Kusini ndilo ambalo lina vijiji vingi vinavyopakana na nchi ya Congo kwa maana ya ukanda wote wa Kalemi. Hadi leo nilikuwa nawasiliana na *DMO,* hakuna kituo hata kimoja ambacho kimewekewa mashine ya kuwapima Wakongo wanaotumia maboti kuingia nchini kwetu.

Je, Wizara imejipangaje kuisaidia Halmashauri ya Uvinza, wananchi wake wasiathirike na huu na ilhali wameingiliana kwa kiwango kikubwa sana na nchi ya Congo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kusisitiza kwamba sisi kama Serikali tumeendelea kujipanga, siyo tu katika sekta za afya, tunashirikiana na mamlaka nyingine za Kamati za Ulinzi na Usalama na zimepewa elimu hii kuhakikisha kwamba katika maeneo ambayo tuna mipaka, tunaweka ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, timu yetu ya Wizara kupitia Mganga Mkuu wa Serikali, hivi tu juzi ametoka tena Kigoma kwenda kukaa na kufuatilia

kuhakikisha haya tunayoyasema wakiwa pamoja na Shirika la Afya Duniani kwenda kuangalia jitihada na juhudi ambazo tunaendelea kuvifanya. Niseme tu kwamba mipaka yetu iko salama, tutaendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yake nyingine ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge, kuhusiana na kuweka huduma za ufuatiliaji wa wagonjwa katika Vituo vyetu na Zahanati, hatuwezi tukaweka katika maeneo yale. Ugonjwa huu ndugu zangu ni hatari sana. Sio kila mtu anayeruhusiwa kumgusa wala kumtibu mgonjwa huyo. Pale anapobainika, watoa huduma wetu wamepewa maelekezo jinsi gani ya kum-*handle* na kum-*isolate* yule mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ambazo zina uwezo zaidi ambazo ni zile *Isolation Centers* zetu na maabara zile ambazo tumezitenga, ndiyo ziweze kuchukua majukumu ya kumtibu yule mgonjwa. Sio kila mtu ana uwezo wa kuwatibu wagonjwa hao. Kwa hiyo, nilitaka nimhakikishie tu kwamba mipaka yetu iko salama, na sisi kama Serikali, tumejipanga vizuri.

**MWENYEKTI:** Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliopo katika Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Mheshiimiwa Ali Davutoglu, Balozi wa Uturuki nchini Tanzania. *Welcome to the Parliament in Dodoma*. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 14 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni viongozi kutoka Kampuni tano za Dawa na Vifaa Tiba kutoka nchini China wakiongozwa na Ndugu Shi Feng. *Welcome to the Parliament*. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Stella Ikupa, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya watu

wenye ulemavu ambao ni Ndugu Mosey Feka kutoka Morogoro, mwingine ni Janeth Mbilinyi kutoka Dar es Salaam na Ndugu Gibson Gondwe kutoka Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Gibson Meiseyeki ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Pwani, karibuni. Vilevile tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wapigakura wake kutoka Mkoani Songwe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Rashid Shaban na Ndugu Francis Daudi. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambao ni viongozi wa Kanisa la *SDA* kutoka Muheza Mkoani Tanga wakiongozwa na Mzee wa Kanisa, Ndugu John Mdoe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanakwaya kutoka kanisa la EAGT Frelimo Mkoani Iringa. Karibuni. Pia tunao *w*ageni wanne wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao ni familia yake kutoka Makambako Mkoani Njombe. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Huu Muswada tunaumaliza sasa hivi. Natoa miongozo miwili; mmoja huku na mmoja huku.

Mheshimiwa Susan na Mheshimiwa Mlinga.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Moja ya kazi kubwa ya Bunge ni pamoja na

kutunga sheria. Natambua kwamba Kiti chako kilishatoa utaratibu wa jinsi ya kuleta *amendments,* lakini mimi na wewe tumekuwa huku Bungeni kwa muda mrefu na hata Mheshimiwa Jenista anaelewa kwamba ilikuwa Wizara inapoleta muswada, siku ile ile ya kwanza wanaleta na *amendments* zake ili Waheshimiwa Wabunge wanapochangia wasiwe wanarudia mambo ambayo tayari yamewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu mpaka sasa hivi tunavyozungumza, Serikali haijaleta mabadiliko yoyote. Sasa swali langu, ni kwa nini hali hii inaendelea au Serikali inataka kuchukua *amendments* za Waheshimiwa Wabunge halafu waingize au ni nini? Kwa nini utaratibu wa zamani usiwepo Serikali ilete mabadiliko yake wakati wanapo-*present* siku ya kwanza ili tusiogelee maeneo ambayo tayari Serikali imesharekebisha?

Mheshimwia Mwenyekiti, ahsante na naomba Mwongozo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Naomba Mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) ambayo inatokana na swali namba 34 linalohusu miradi ya barabara. Sasa hivi ninavyoongea, nchi nzima miradi mikubwa ya barabara na ujenzi ambayo inafadhiliwa na wafadhili imesimama. Kwa nini imesimama? Iimesimama kutokana na wakandarasi kususa kufanya kazi hiyo kwa sababu ya mkanganyiko wa kodi ya *VAT* yaani Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa sababu Wizara ya Fedha ni Serikali na Wizara ya Ujenzi ni Serikali, wamekuwa wakiogopana kama mtu na baba mkwe wake kiasi cha kwamba wanasababisha wananchi tunakosa huduma.

Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako, kwa sababu wote wako ndani humu na Bunge kazi yake kuisimamia Serikali, wakae mpaka saa 7.00 mchana watupe majibu, kwa nini miradi ya barabara inakwama kutokana na mkanganyiko wao wenyewe, Serikali kwa Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni. Nipeni muda nitawajibu. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018** ***(The Tanzania Teacher's Professional Board Bill, 2018)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaanza na Mheshimiwa Kandege kwa dakika 15.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya kuweza kuchangia…

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ehe, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona unaanza kuita Mawaziri, lakini kama tulivyokuwa tumearifiwa jana na ilivyokuwa kwenye *Order Paper,* huu muswada unajadiliwa kwa siku mbili. Jana tulitoka mapema na leo bado muda upo. Sasa tunaomba ufafanuzi, ni kwa nini muswada huu unahitimishwa mapema wakati kuna wachangiaji wa kutosha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini nilishakujibu asubuhi. Sijaona sababu ya kuuliza tena. Nilishakujibu asubuhi na majibu unayo kwenye meza yako.

Mheshimiwa Kandege. Nime-*deal* na *Chief Whip* asubuhi. Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukushukuru kwa fursa ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania kwa mwaka 2018. Nina kila sababu ya kuishukuru Wizara kwa kuleta muswada huu ambao kimsingi umechelewa. Muswada huu ulitakiwa uwe umefika mapema. Ziko sababu za wazi kabisa kwa nini nasema muswada huu umechelewa katika kuletwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *composition* ya wafanyakazi walio wengi Tanzania ni walimu. Kwa wingi wao huu walikuwa wanahitaji wawe na chombo ambacho kitawasemea, kita-*regulate* na kuhakikisha kwamba kazi ya ualimu inarudi hadhi yake kama ambavyo ilikuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna kazi ambazo zilikuwa zinaheshimika sana ilikuwa ni pamoja na kazi ya ualimu. Sasa hapa katikati imefika mahali ambapo kama vile mtu akikosa kazi ya kufanya, kazi ya mwisho ya kukimbilia ni ualimu. Sasa kwa muswada huu ambao naamini Bunge lako tukufu litaenda kupitisha na kuwa sheria, maana yake hadhi ya walimu Tanzania imeanza kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michango ambayo imetolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakiwa wanataka kuoanisha suala la kuletwa kwa muswada huu na madai ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashuhuda jinsi ambavyo Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba madai ya walimu yale yote ambayo yamehakikiwa yanalipwa. Kwa

hiyo, hatuwezi tukasema kwamba eti kwa sababu walimu wana madai yao ndiyo tusianzishe chombo ambacho kitakuwa kinawasimamia na kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ni shuhuda, katika *professions* nyingi ambazo zinaheshimiwa ni zile ambazo zina Bodi zake ambazo zina-*regulate.* Ukienda kwa upande wa sheria, kiko chombo ambacho kinaweka pamoja *learned brothers and sisters* na wamekuwa na taratibu namna ya kuweza kumtambua mwanasheria. Kuna sheria ambazo wanawekeana taratibu na huwa wanafanya kukutana kila mwaka wakijadili mambo yao. Naamini hii itakuwa ni fursa nzuri sana kwa walimu na wao kuweza ku-*adress* mambo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, utakuta hata kwa mfano Bodi ya Wahandisi ipo na sasa hivi wako Dar es Salaam wakifanya mkutano wao wa mwaka wakiadhimisha miaka 50 tangu wameanzisha. Kwa hiyo, suala la kuwepo kwa Bodi ya Walimu ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna madai kwamba tungeanza kuangalia habari ya miundombinu. Wewe na Waheshimiwa Wabunge wote ni mashuhuda. Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikihakikisha kwamba miundombinu inaendelezwa, inajengwa na vyumba vya madarasa vinaongezwa. Suala zima la nyumba za Walimu nalo linawekewa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, hivi karibuni tulishuhudia suala la kugawa pikipiki kwa kata zote Tanzania. Tafsiri yake ni nini? Tunataka hawa ambao wamegawiwa hivi vyombo vya usafiri iwarahisishie ili wakati tunadhibiti ubora wa elimu kusiwe na kisingizio na pale inapatikana posho ya shilingi 200,000 kwa ajili ya hivi vyombo kuhakikisha kwamba watu wetu kwa maana ya Waratibu Elimu wanapata fursa ya kwenda kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna fursa ambayo Walimu wamekuwa wakikosa ni pale ambapo inatokea hata fursa ya kwenda kufundisha lugha yetu ya Kiswahili, Walimu wetu wako bora kabisa katika suala zima la kufundisha lugha ya Kiswahili. Ukilinganisha na nchi jirani kwa sababu hakuna chombo ambacho kinatoa udhibiti na kuweza ku-*regulate...*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu. Serikali inajibu na majibu yenu yanapatikana sasa hivi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** ... kwamba huyu tutawezaje kumthibitisha kama ni mwalimu kama hakuna chombo ambacho kina-*regulate* na kiko *specific* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mwalimu ambaye ameingia huko, isiwe kama vile ambavyo amekosa kazi zote, mtu kamaliza *form six* sasa anakusanya darasa anaanza kufundisha. Kwa hiyo, ni ngumu sana kuweza kuwa na *professionalism* na hili ndiyo kubwa zaidi kuliko mambo mengine yote. Tukiwa na hao watu ambao wanatambulika na *professionals* zao ni rahisi sasa hata kushughulikia matatizo yao na kuboresha hali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la *capacity building,* imesemwa hapa kwamba kwanza tuwajengee uwezo. Kwa Serikali ya Awamu ya Tano suala la kujengea walimu uwezo limekuwa ni kipaumbele na kwa kadri bajeti inavyoruhusu tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo ili walimu wetu wafanye kazi yao kwa weledi na kuhakikisha kwamba elimu bora tunayoitarajia kwa watoto wetu ndiyo inayotolewa. Hili linawezekana pale tu ambapo wao wenyewe kwa kuwa na Bodi ambayo na wao watashiriki katika kuhakikisha kwamba taratibu na kanuni ambazo zitaweza ku-*identify* wao kama walimu, itakuwa ni rahisi hata masuala ya kinidhamu wao wenyewe kuweza kuji-*regulate.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba chombo hiki walipigana sana akina Mheshimiwa Mama Sitta kilitakiwa kiwe kimeshaanzishwa muda mrefu.

Ni matarajio kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao tuna nia njema na Serikali yetu na elimu yetu ambayo tunataka iweze kushindana, ni vizuri tukahakikisha kwamba tuna-*support* ili chombo hiki kiweze kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nikushukuru kwa fursa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkuchika, ajiandae Mheshimiwa Ole-Nasha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini nieleze kwamba mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taaluma mimi ni mwalimu. Nilikuwa naona wivu sana wenzetu wa taaluma nyingine bodi kama hizi wanazo siku nyingi, tena wao wachache kuliko sisi walimu, ndiyo maana nikasema kwamba pengine hoja hii imechelewa, ndiyo maana nikasema ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameeleza umuhimu wa kuwasajili walimu. Ndiyo maana nasema kama zoezi hili limechelewa, sio sisi wa mwanzo, Wakandarasi wanayo Bodi, Madaktari wanayo Bodi, Wauguzi wanayo Bodi, Wafamasia wanayo Bodi, sasa katika watumishi wa Serikali ambao mimi ndio Waziri wao, watumishi wengi wa Serikali ni walimu. Kwa hiyo, kukaa muda mrefu bila kuwa na chombo kama hiki, tumechelewa. Ndiyo maana nikasema mimi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mawaziri tunahudhuria Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna jambo wanaita *harmonization,* wanataka muhtasari wa masomo yote katika nchi mbalimbali ufanane ili mwalimu aliyehitimu Rwanda aweze kufundisha nchi yoyote, lakini ili uweze kwenda kufundisha nchi nyingine lazima uwe umesajiliwa katika nchi yako. Leo sisi tunahitaji walimu wengi wa kwenda kufundisha

Kiswahili nje, lakini kwa kukosekana hili huwezi ukatambua mwalimu gani ana sifa ya kufundisha Kiswahili nje ya nchi. Bodi ikishafanya kazi yake itakuwa ni muda muafaka sana wa kuweza kuwasajili ili waweze kutambulika kwa urahisi huko nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa imetolewa hoja ambayo siafikiani nayo kwamba muswada unakusudia kuwadhibiti walimu. Mimi nasema mtumishi yeyote wa umma aliyeajiriwa kuna kiwango cha kudhibiti ndiyo maana kunawekwa sheria, taratibu na kanuni, ile unamdhibiti mtumishi. Hata mtu binafsi akimwajiri mtu, yule aliyemwajiri anampa miiko ya ile kazi, sasa sembuse mwalimu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kusema jamani, hakuna mtu muhimu katika historia yetu sisi wote kama mwalimu. Ndiyo maana wanasema mwalimu ndio mzazi wa pili, kwa nini? Mtoto akizaliwa, amekua, anapata malezi kwa baba na mama. Baada ya pale anamkabidhi yule mtoto kwa mwalimu, ndiyo maana mwalimu lazima awe ana nidhamu ili yule mtoto afuatishe nidhamu ya mwalimu. Ndiyo maana taaluma hii ya ualimu kweli kama bodi tunayoiunda itasaidia kudhibiti mwenendo na tabia ya walimu, mimi naunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano, mimi nimesoma Arusha, shule moja inaitwa Ilboru, nilikwenda pale *form five* na *six.* Nimekuta shuleni kuna kitu kinaitwa *Ilboru Personality.* Moja, marufuku kwenda mjini kununua karanga umevaa *uniform* ya shule unatafuna karanga huku unatembea. Ukifanya hivyo, wanafunzi wenzako wanakuchora, akikuona mwalimu anakuchora, Jumatatu unapewa adhabu na unatangazwa kwenye *assembly* kwamba huyu *weekend* hii aliharibu heshima ya *Ilboru Personality.* Alitafuna karanga barabarani akiwa anatembea, alinunua mahindi akawa anatembea barabarani. Pakawa pana nidhamu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani sisi tuliosoma tulikuwa tunaangalia mwalimu amevaaje? Amenyooshaje

nguo yake? Nguo yake ni nzuri kiasi gani? Kwa sababu mwalimu ni kioo cha mwanafunzi. Kwa hiyo, tusiwe na hofu hapa ya kusema kwamba watakuwa walimu wanadhibitiwa, hapana. Lengo ni kwamba tufanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naikubali sana hoja iliyotolewa hapa na ndugu yangu, Mheshimiwa Hongoli, anasema kwamba hatuwezi kukubali walimu wanavaa hovyo. Nimesema hapa, na mimi namuunga mkono. Mwalimu akivaa hovyo, mtoto naye atavaa hovyo.

Mimi nilikwenda kwenye sherehe moja, Siku ya Walimu Duniani, sitaki kusema ni mkoa gani au wilaya gani, nikawa mgeni rasmi. Yule waliyemleta kuja kusoma risala hakuchana nywele. Katika mazungumzo yake akasema;"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya" maana nilikuwa Mkuu wa Wilaya. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, walimu tuna hali ngumu, mishahara midogo na nini na nini, wenzake wakampigia makofi ukumbi mzima. Mimi nikamuuliza, je, na kutochana nywele nako hapo, nayo ni hali ngumu ya uchumi? Mwalimu ana heshima yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtaalam wa lugha. Nilifaulu somo linaitwa *english literature,* tukasoma mambo ya akina *Shakespeare,* nilipata *one distinction,* nilishinda kuliko watoto wa Malkia. Walimu wakaniambia niende nikasomee uanasheria, maana kweli ningeweza. Huku *literature,* huku *history* nikapata *two,* kiswahili nikapata *three.* Nilipokwenda Chuo Kikuu nikaambiwa wewe ni mtu wa sheria. Nilipomwambia baba yangu, akaniambia sitaki, nataka ufanye kazi ya heshima. Kazi gani? Ualimu. Nika-*comply,* nikaenda kusomea ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba bodi hii ambayo tumeiunda itasaidia sana kuinua kiwango cha utendaji kazi wa walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja hapa; nataka nieleze tu jinsi walimu wanavyoshughulikia upande

wa madai ya malimbikizo ya mishahara. Serikali imeweza kulipa jumla ya shilingi bilioni 45 kama malimbikizo ya mishahara ya kwa watumishi 27,437 baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa watumishi hewa na vyeti vya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malipo hayo, jumla ya walimu 15,000 walilipwa jumla ya shilingi bilioni 16. Nataka niwahakikishie walimu, ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba malimbikizo ya madai ya walimu yanakuwa historia na mwaka huu tutaendelea kumaliza matatizo yote yaliyobaki kwa madai ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa upandishwaji vyeo, nataka nieleze tu kwamba baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki, jumla ya watumishi 44,275 wakiwemo walimu 28,000 wamepandishwa vyeo na taarifa zao kuidhinishwa kwenye Mfumo wa *CHMIS* kuanzia mwezi Novemba, 2017 hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa juu ya uhaba wa walimu na mimi nakubali. Uhaba tulionao kwa watumishi, siyo walimu tu, katika fani nyingine zote, lakini tunachotaka kusema, tunapoajiri tunawapa walimu kipaumbele kwa umuhimu wao, ndiyo maana mmeona tumekuwa tunaajiri sana walimu wa masomo ya *arts,* baadae ilipoonekana wamekuwa wengi, wamepelekwa kwenda shule za msingi, lakini na juzi hapa tumeanza kuajiri walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo hapa ni kwamba idadi ya walimu wa sayansi na walimu wa *arts* iwe sawa. Hakuna anayesema kwamba masomo ya *arts* ni muhimu kuliko sayansi wala sayansi muhimu kuliko *arts* kwa sababu yote hayo yanahitajika. Tunahitaji wanasheria na ma-*engineer* wote wanahitajika. Huwezi ukawa pande zote kama hujasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kati ya nafasi za ajira mpya 52,436 kwa mwaka 2017/2018 kada ya elimu ilitengewa jumla ya nafasi 16,000 hadi sasa jumla ya walimu 6,840 wameshaajiriwa na kugawanywa kwenye vituo vyao mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2018 Serikali imepanga kuajiri watumishi 49,000 wakiwemo na kada ya ualimu. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, tutakapokuwa tumetoa ajira kwa walimu kama tulivyokusudia tunaamini kwamba, uhaba wa walimu utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yalikuwa yanahusu Wizara yangu, yaliyoguswa katika mjadala hapa ndani naona kama nimeyajibu. Nirudie kukushukuru tena kueleza kwamba, naunga mkono hoja, tuwape walimu hadhi yao kama tulivyowapa hadhi ma-*engineer,* tulivyowapa hadhi wanasheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Ole-Nasha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi na mimi niweze kuchangia muswada uliopo mbele yetu. Ninaomba kwanza kutumia nafasi hii kuashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa kweli, wametumia muda walioupata vizuri kuchangia muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda ambao tutapata hatutaweza kujibu hoja ya kila Mbunge, lakini tumejitahidi sana kadri ya kama mtakavyoona kwenye Jedwali la Marekebisho kuchukua mengi ya yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nieleze tu kwamba kwa kweli muswada huu umechelewa sana kwa sababu, wadau mbalimbali kwa muda mrefu sasa wamekuwa

wakizungumzia umuhimu wa kuwa na sheria maalum itakayolinda hadhi ya taaluma ya walimu. Kwa sasa katika nchi yetu mtu yeyote yule ambaye anajua kushika chaki, anavaa suruali, anavaa sketi, anaweza akaenda darasani na akaitwa mwalimu. Kitendo hiki kwa muda mrefu sasa kimefanya taaluma ya ualimu isionekane kwamba ni taaluma. Ukweli wa mwambo ni kwamba ualimu ni taaluma inayosomewa, inayobobewa, yenye hadhi, kwa hiyo haiwezekani kwamba mtu yeyote yule ambaye hajasomea wala hajabobea akajiita mwalimu. Kwa hiyo, sheria hii imekuja ili kulinda heshima hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wa nchi yetu kama unazungumzia kuhusu wanataaluma tulionao kama nchi wengi wao ni walimu. Tunao zaidi ya walimu 300,000 katika nchi hii, lakini wao pekee kati ya taaluma nyingi tulizonazo ndiyo hawana chombo ambacho kinalinda heshima ya taaluma. Kwa hiyo, walimu na wananchi wote watuunge mkono kwa sababu lengo kubwa ni kulinda heshima ya taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameonesha/wametoa michango kuhusu maeneo mbalimbali na ningependa kutumia muda mfupi kujaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo wamezileta. Nikianza na yale yaliyoletwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni walizungumzia kuhusu chimbuko la muswada huu, kwa maoni yao wao waliona kwamba Serikali ilisema kwamba chimbuko lake lilikuwa ni Waraka wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wa mambo ni kwamba chimbuko la muswada huu ni wananchi na wadau mbalimbali ambao kwa kipindi kirefu sana wao wenyewe wameona mapungufu ambayo yapo katika sekta ya elimu na wakashauri kwamba njia mojawapo ya kuboresha elimu ni kuwa na sheria itakayolinda hadhi ya taaluma ya walimu. Kwa hiyo, kwamba imepitia kwenye Baraza la Mawaziri ni

utaratibu wa kawaida wa kutunga sheria, lakini ukweli wa mambo chimbuko lake ni wananchi na ni wadau mbalimbali wa sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyokumbuka hata wenyewe kwa muda wa miaka mitatu sasa mfululizo mmekuwa mkisisitiza kwamba tulete muswada huu Bungeni. Nakumbuka wakati wa mjadala wa bajeti yetu iliyopita mmetushikia hata shilingi kwamba usipoleta hatutapitisha bajeti yenu, tukasema tutaleta. Kwa hiyo, kwa kweli sisi kama Wizara, sisi kama Serikali tumeridhia mapendekezo yenu na ndiyo maana tumekuja na huu muswada. Kwa hiyo, kwa kweli chimbuko ni mjadala ambao umekuwa ukiendelea na sio Serikali imeleta yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni vilevile ilionesha wasiwasi kwamba kuletwa kwa Bodi hii ya Kitaaluma ya Walimu inaweza ikaongeza ukubwa wa matumizi ya Serikali. Ni kweli kwamba, Bodi hii itakuwa na gharama, lakini faida zake tukiziangalia kwa kweli, faida zake ni nyingi kuliko gharama ambayo tutatumia katika uendeshaji wa bodi ambayo inaanzishwa. Hata hivyo kama mtakavyoona kwenye Jedwali la Serikali la Marekebisho kwa kweli, tumejaribu kupunguza gharama zozote ambazo zinaweza zikaongezeka kutokana na uanzishwaji wa bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni vilevile wameweza kuonesha wasiwasi kwamba kuletwa kwa Bodi hii ya Walimu itaongeza mzigo wa michango kwa walimu nchini. Tumepitia kwa umakini sana pendekezo hilo na kama mtakavyoona tumeweza kupunguza tozo mbalimbali ili kuondoa gharama ambayo inaweza ikawapata walimu. Kwa hiyo, tunawaondolea wasiwasi kwamba haitakuwa na gharama kubwa, vilevile gharama ambazo zitakuja kutungwa kwenye kanuni ambazo zitaletwa baadae na Waziri kwa mujibu wa sheria, vilevile zitashikisha walimu wenyewe na wadau wengine, ili tuhakikishe kwamba, haileti mzigo wa ziada kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mjadala vilevile kwamba, muswada huu utakuja kuwadhibiti walimu. Ukweli wa mambo muswada huu lengo lake siyo kuwadhibiti walimu, lakini ni kudhibiti uholela kwenye taaluma ya ualimu. Kwa hiyo, kwa wale ambao hawataendana na masharti na miiko pamoja na maadili ya ualimu kwa kweli watadhibitiwa kwa sababu tunataka tulinde hadhi na heshima ya taaluma ya ualimu kwa hiyo, ni lazima wale ambao hawataendana na matakwa sasa ya sheria lazima watadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema kimsingi ni kwamba tukiacha ualimu uendelee kuendeshwa kiholela maana yake tutaendelea kukubali watu ambao hawana taaluma wala hawana maadili kufundisha kwenye shule zetu na hivyo kuendelea kusababisha kushuka kwa kiwango cha elimu. Kwa hiyo, tunaamini kwamba unapofanya udhibiti walimu wanaofundisha kuwa ni wale ambao wametambuliwa kisheria, lakini vilevile ambao wanafuata maadili tunaamini itatusaidia katika jitihada zetu za kuendelea kuboresha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wabunge ambao walionesha wasiwasi kwamba, muswada umetoa madaraka makubwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa sababu, anaonekana kufanya teuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na uteuzi ule wa Mwenyekiti wa Bodi ya Taaluma ya Walimu. Kama nilivyosema tumejaribu kupunguza baadhi ya madaraka ambayo amepewa Waziri katika muswada huu, ikiwa ni pamoja na kuleta pendekezo la kuwa Mwenyekiti sasa wa Bodi atateuliwa na Rais. Kwa hiyo, tumefanyia marekebisho baadhi ya vipengele kama mtakavyona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge vilevile walionesha wasiwasi kwamba bodi ile haijashirikisha sana sekta binafsi.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumefanya marekebisho makubwa ili kuleta kwa ukubwa zaidi ushiriki wa sekta binafsi katika uendeshaji wa bodi. Baadhi ya Wabunge vilevile walikuwa na wasiwasi

kwamba, walimu katika muswada ule hawajapatiwa fursa ya kukata rufaa endapo hawataridhika na maamuzi ya bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kuwa muswada umeweka bayana kwamba kama mwalimu haridhiki na uamuzi wowote wa bodi anapewa fursa ya kukata rufaa kwa Waziri, vilevile inazungumzia kinagaubaga kwamba vilevile atakuwa na haki ya kwenda kwenye Mahakama Kuu. Kwa hiyo, suala la rufaa limetiliwa maanani katika muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge baadhi yao wamezungumzia kuhusu umuhimu wa kuwa na mjadala wa kitaifa kuhusiana na maadili ya ualimu. Ushauri umezingatiwa na ni kweli kwamba kwa sasa tunafahamu kuhusu baadhi ya maadili ya walimu, lakini tunakiri kwamba, siyo vibaya huko mbele tukawa na uelewa wa pamoja kuhusu maadili ambayo yanategemewa kwa kila mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndalichako, Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kujadili hoja hii tangu jana nilipoiweka hapa mezani na hata sasahivi ambapo tunahitimisha. Nakushukuru wewe kwa kutuongozea vema mjadala wetu na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao hakika niseme kwamba hoja hii imepokelewa vizuri sana na Wabunge wote na kimsingi Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wameiunga mkono hoja hii, lakini wamekuwa tu maeneo machache ambayo wametoa mapendekezo ili Serikali iweze kuangalia na kuweza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niishukuru tena Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Serukamba kwa ushirikiano mkubwa ambao ameutoa tangu Serikali ilipowasilisha muswada huu. Hakika Kamati imefanya kazi kubwa, wamechambua Taarifa ya Kamati iligawiwa Bungeni jana, mmeona ni jinsi gani Kamati kwa kweli imeutendea haki huu muswada, sisi Serikali tunasema tunashukuru sana, asilimia kubwa ya maoni ambayo yametolewa na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Serikali imeyapokea na mtayaona tutakapokuwa tunapitia kifungu kwa kifungu tumeweza kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Pia nashukuru upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia kwa maoni yao ambayo wameyatoa na mengine Serikali imeweza kuyazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ilichangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 20 ambao walionga na Wabunge kumi ambao wamechangia kwa maandishi.

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo kwa kweli michango yote ilikuwa inalenga katika kuhakikisha kwamba tunatengeneza chombo ambacho kitaenda kuisaidia nchi yetu kuhakikisha kwamba mwalimu anakuwa na hadhi, pia upande mwingine kitahakikisha kwamba hakuna suala ambalo labda litakuwa linaongeza gharama na michango kwa walimu ambayo itakuwa inawapa mzigo. *(Makofi)*

Kwa kuwa kanuni haziniruhusu kutaja majina ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, basi niseme tu kwamba, orodha yao ya majina ninayo hapa na nitaomba iingie kwenye *Hansard.*

Orodha ya Majina ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania, 2018 kwa kuzungumza na maandishi kama yalivyowasilishwa Mezani:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mheshimiwa Othman Omary Haji, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Maghembe, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mheshimiwa Richard Phillip Mbogo, Mheshimiwa Balozi Dkt. Deodoriou B. Kamala, MheshimiwaEdward F. Mwalongo, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Almas Athuman Maige na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mheshimiwa Zainabu Mndolwa Amir, Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakar, Mheshimiwa Omar Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola na Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kwanza niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wametangulia na wameweza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja na vipengele ambavyo vilizungumziwa na wachangiaji ambao wamezungumzia muswada huu. Kwa hiyo, nashukuru kwa michango yao na ningependa kujikita katika kuzidi kuweka msisitizo wa madhumuni ya kuanzisha Bodi ya Utaalamu wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mkanganyiko kwamba sasa hii inakuwa inasababisha walimu wanakuwa na vyombo vingi vya kuwahudumia na kwamba Bodi ya Utaalam wa Walimu inaenda kuchukua kazi za Tume ya Utumishi wa Walimu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hakuna muingliano wowote wa kimajukumu kwa sababu Tume ya Utumishi wa Walimu iko chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na jukumu lake

ni kuangalia utumishi wa walimu katika sekta ya umma. Kwa hiyo, wao wanajikita katika kuangalia masuala ya kiutumishi na katika Tume ya Utumishi wa Walimu walimu wanakuwa kuna kumbukumbu kama ambavyo hata hapa Bungeni bila shaka kunakuwa na kumbukumbu ya kuonesha kwamba, Bunge lina Wabunge wangapi, kutoka Jimbo lipi na kadhalika. Kwa hiyo, ile *register* ambayo inatunzwa na Tume ya Utumishi wa Walimu ni kwa ajili ya taarifa za kumbukumbu za kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bodi ya Utumishi wa Walimu tutaweka *register* ambayo itatuwezesha kutambua walimu walioko nchini katika sekta ya umma, katika sekta binafsi, pia itakuwa inatambua hata walimu ambao ni wageni kutoka nje ya nchi. Tume ya Utumishi wa Walimu inasimamia nidhamu ya walimu kiutumishi. Ukiangalia hata Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye masuala ya nidhamu inasema kwamba masuala ya nidhamu ya kiualimu yatazingatia taratibu za utumishi wa umma. Sasa katika Bodi ya Utaalam wa Walimu tunataka kuangalia zaidi katika maadili na miiko ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hakuna mtu ambaye hafahamu umuhimu na thamani ya mwalimu. Mwalimu ni kioo cha jamii, mwalimu ni mtu ambaye anakaa muda mwingi na watoto wanapokua katika umri wa kwenda shule kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Ukiangalia saa ambazo watoto wanakaa shuleni ni nyingi zaidi kuliko hata yale ambayo wanakaa na wazazi. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba tunalinda maadili, haiba ya mwalimu, utendaji wake na muonekano wake katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Bodi ya Utaalam wa Walimu ambayo tunaiunda itakuwa pia inaangalia miiko na maadili ya walimu. Kwa hiyo, hata masuala ya mavazi, nafahamu kwamba hata masuala ya mavazi kwenye utumishi wa umma yameainishwa, lakini hapa tunataka kuweka msisitizo zaidi ili hata zile adhabu zinazotolewa kwa sababu makosa katika utumishi wa umma yameweka pamoja na

adhabu, lakini pengine kutokana na umuhimu wa walimu kuna makosa mengine ambayo yanadhalilisha taaluma ya walimu. Tunataka kuhakikisha kwamba yale makosa ambayo yanashusha hadhi ya ualimu yanakuwa yanashughulikiwa na bodi ambayo imeundwa mahususi katika kuangalia utaalamu wa ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wamezungumza waliokuwa wanajibu hoja waliotangulia ni kwamba, hata taaluma nyingine zinazo bodi zao ambao zinasimamia. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba tumechelewa sana kuanzisha Bodi ya Utaalamu ya Walimu kwa sababu wenzetu wahandisi jana walikuwa wanasherehekea miaka 50 ya Bodi ya Makandarasi, lakini leo hii walimu ambao ndiyo fani ambayo ni muhimu, hata hao makandarasi wasingeweza kufika hapo bila kuwa na mwalimu. Kwa hiyo, ualimu ni fani ambayo kwa kweli, ndyo taaluma mama kwa sababu, walimu ndiyo wanazalisha hata hizi *profession* nyingine ambazo tayari zimekuwa na bodi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo mmekuwa mkiunga mkono wakati wa uchangiaji naomba kabisa hata tutakapokaa katika *session* ya kupitia kifungu kwa kifungu muendelee kuunga mkono ili hatimaye hili jambo ambalo kwa kweli lilikuwa limechelewa basi liweze kupitishwa na tuweze kuanza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge katika michango kuna jambo ambalo wengi waliokuwa wanazungumza walionesha wasiwasi wa tozo zinazotolewa na kwamba kutakuwa na ada ya usajili, kwamba Serikali inakwenda kumbebesha mzigo mwalimu, ukiangalia kipato chake na hali halisi ya maisha.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la tozo, suala la ada kwa kweli, Serikali haikusudii hata kidogo kumpa mwalimu mzigo wa ziada. Baada ya kusikiliza maoni na mapendekezo mtaona katika jedwali letu hata zile tozo za adhabu kwa kweli, tumezipunguza kwa kiasi kikubwa. Niwahakikishie kwamba

baada ya huu muswada kupitishwa ni kwamba tutatunga kanuni na kanuni zitakapokuwa zinaandaliwa zoezi la uandaaji wa kanuni litakuwa ni shirikishi. Kwa hiyo, ada itakuwepo, lakini itakuwa ni kiasi kidogo sana ambacho hakuna mwalimu ambaye ataweza kushindwa, lakini pia haitakuwa ni suala ambalo litakuwa ni mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaona katika marekebisho ambayo tumeyaleta kwa kweli, hili suala tumelizingatia sana, lakini niwahakikishie kwamba hata katika hatua ya kutengeneza kanuni tutahakikisha kwamba suala la gharama linazingatiwa kwa sababu si lengo la Serikali kumpa mzigo mwalimu kwa sababu tunathamini kazi ya ualimu na tungependa kwa kweli walimu waendelee kulitumikia Taifa hili kwa moyo wao wote. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile Serikali isingependa kuwapa mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni kwamba uwakilishi wa Vyama vya Walimu katika Bodi na kwamba kuwe na uwakilishi katika muundo wa bodi na kadhalika. Niseme kwamba suala hili limezingatiwa na imekuwa ni vigumu kwa Serikali kuweza kutaja kwamba labda ni chama gani cha walimu kitaingia kwa sababu hata walimu wenyewe hawana chama kimoja, kuna Chama cha Walimu Tanzania, kuna chama kinachotetea haki na maslahi ya walimu. Kwa hiyo, hata walimu kama wao hawana *umbrella* moja au hawana chama kimoja ambacho kinatetea maslahi yao. Sisi kama Serikali kwa sababu vyama vyote vimeanzishwa kisheria tutakachokifanya vyama vyote vitakuwa vinatambuliwa na unaweza hata ukawekwa utaratibu kama itakuwa ni kwa *rotation,* lakini kitu kikubwa ambacho tutazingatia ni sifa za mtu ambaye anateuliwa kuingia katika bodi. Jambo la msingi kwa sababu ni suala la uwakilishi na ni suala la majukumu kwamba anakuja kutekeleza jukumu fulani, kwa hiyo, uwakilishi katika vyama vya walimu utazingatiwa, lakini kubwa zaidi itakuwa ni weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie pia hata katika suala la uteuzi wa Wajumbe wa Bodi na pia suala la

uadilifu na suala la weledi na utaalam kwa sababu anakuja kusimamia utaalam wa walimu. Ni dhahiri kwamba mtu ambaye anapaswa kufanya hivyo lazima kwanza yeye mwenyewe awe amethibitika bila shaka kwamba amefuzu na ana vigezo vinavyotakiwa lakini pia hata na uadilifu wake usiwe unatia shaka, kwa sababu wewe huwezi ukasimamia maadili ya wenzako wakati na wewe uadilifu wako unatiliwa shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba suala la uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ni kuhakikisha kwamba wanateuliwa kwa kuwakilisha zile taasisi zote ambazo zinamhusu mwalimu utaona katika ile *composition* tumependekeza hata hii Tume ya Utumishi wa Walimu wawepo ndani ya Bodi na kama kutakuwa na kujitokeza jambo lolote huko mbele ambalo labda litakuwa na muingiliano basi yule Mjumbe kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu anaweza akawa analiona na kuliratibu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba naomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono muswada huu ambao madhumuni yake makubwa ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia hadhi na viwango vya ubora wa walimu katika nchi yetu na kutoa leseni kwa walimu wote walio katika sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ambayo tutaipata kutokana na muswada huu, muswada huu unaweza ukamzuia mwalimu ambaye anafukuzwa kazi kwa makosa ya kuiuka maadili katika utaratibu wa sasa Tume ya Utumishi wa Walimu inamuondoa kwenye *register,* lakini mwalimu huyu anaweza akaenda akafundisha shule binafsi wakati anawafundisha watoto wa Kitanzania.

Kwa hiyo, sasa hivi kupitia Bodi ya Utaalam wa Walimu mwalimu ambaye ataonekana kwa kweli hana maadili ambayo yanaendana na fani ya ualimu akiondolewa kwenye bodi hataweza kufundisha mahali popote kwenye Serikali au binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi itaandaa *code of professional conduct* yaani itakuwa inasimamia maadili ya utaalam wa walimu wakati Tume ya Utumishi wa Walimu inasimamia maadili ya walimu kama watumishi wa umma na imejikita tu kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakuna mtu asiyefahamu changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika shule binafsi. Hakukuwa na sheria ambayo inabana moja kwa moja viwango na maadili ya walimu ambao wanaajiriwa katika shule binafsi.

Kwa hiyo, kupitia sheria hii sasa walimu pia wanaoajiriwa katika shule binafsi, walimu wa shule za awali, shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na taasisi ambazo zinatoa mafunzo ya elimu ya watu wazima wataweza kudhibitiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya ufafanuzi huo sasa kwa heshima kubwa kabisa naomba Waheshimiwa Wabunge wote tutakapokaa kama Kamati kwa pamoja tuunge mkono na kupitisha Muswada huu wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa mwaka *2018 (The Tanzania Teachers' Professional Board Bill, 2018).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Tunaendekea Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa Mwaka 2018 *(The Tanzania Teachers' Professional Board Bill, 2018)***

**MWENYEKITI:** Tukae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baridi limezidi sana humu ndani.

**MWENYEKITI:** Katibu.

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye *clause 3* nimeleta marekebisho ya kuongeza *interpretation* ya *a professional teacher* ambayo ukiangalia kwenye 5(1) inasema kwamba; *a chairman who shall be appointed by the Minister from amongst registered Senior Professional Teachers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja yangu ilikuwa ni kwamba ni lazima kama Serikali itaona inafaa na mimi nadhani inafaa kwamba tuwe na *definition* ya huyu mtu, *actually* nilikuwa nadhani pia na *qualification* zake, lakini walau tujue huyu mtu ni nani, nikasema kwamba huyu mtu sasa sifa zake walau kwa sifa hiyo moja, huyu mtu awe *a professional teacher who has practiced teaching for not less than ten years.*

Kwa hiyo, hilo ndiyo lilikuwa pendekezo langu kwamba hii iwekwe kwenye *interpretation* ili sasa huyu *Chairman* wa hiyo Bodi awe na kigezo hicho kwa sababu anaenda kushughulikia walimu kwa maana hiyo *seniority* iwe walau ina kiwango cha miaka aliyowahi kufanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefikiria sana kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Susan Lyimo lakini tumeona tubakie na *definition* tuliyonayo, kwa sababu tayari kwenye utumishi wa umma tuna madaraja ya ualimu, kwa hiyo leo hii tukianza kutengeneza kwa sheria hii *category* mpya ya mwalimu ambaye anafahamika kwamba ana uzoefu wa miaka fulani, maana yake tayari tumetengeneza daraja ambalo tayari lipo, kwa hiyo ndiyo maana sisi tunapendekeza kwamba ibakie kama ilivyo sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na wazo la Waziri au la Serikali kwa sababu bodi hii pamoja na mambo mengine ni kitu kipya kabisa ambacho kinaleta sekta nyingine ya ualimu ambao pia wanatoka kwenye *private* na kama haya madaraja yapo tunaposema hiyo *seniority* mnamaanisha kitu gani, kwa nini tusiweke kwamba huyu mtu haiwezekani ukasema tu *senior,* mtu anaweza akawa amefanya kazi miaka mitatu au minne akawa ni *senior,* kwa hiyo, tukasema walau kuwe na hiyo *limitation ten years experienced* huyu ndiyo *senior.* Kwa hiyo, *whether* anatoka kwenye *public* au *private.* Maana yake unavyosema hivyo maana yake ni kwamba unataka kutuhakikishia kwamba hamuwezi kumpa mtu wa *private* kwa sababu hajatoka kwenye *public sector* na hii siyo sawasawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema kwamba msimamo wa Serikali tunapendekeza ubaki huo huo kwa sababu kipindi cha kufundisha miaka mitano, kumi, 15 na kadhalika huo ni uzoefu na huo hau-*qualify professionalism. Professionalism* ya mwalimu inatokana na *training,* amepata *professional training,* kwa hiyo, kipindi cha mwaka mmoja, miwili, mitatu hiyo inaitwa uzoefu na hatupendi kuchanganya uzoefu na *professionalism.* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan funga hoja yako.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu kidogo uzoefu maana yake ni nini na *seniority* maana yake ni nini. Kwa sababu ninaamini huwezi kuwa *senior* kama hujawa na *experience* yaani hujafanya kazi, huwezi ukaingia leo kazini halafu ukawa *senior.*

Kwa hiyo, nimeshindwa kumuelewa *AG* kwamba unapata *seniority from what*, lazima upate *seniority* kwa kuwa umeshakaa ofisini au umeshafanya ile kitu kwa muda fulani na hiyo ndiyo *experience.* Hii ndio sababu kuna *junior* na *senior,* haiwezekani mtu amefanya kazi miaka mitatu ukasema huyu ni *senior* kuliko aliyefanya kazi miaka mitano, kwa sababu kama ni *professional* hawa wote lazima wawe nayo *professional* ya ualimu. Kwa hiyo, suala la uzoefu na *seniority* ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema *AG* nadhani anatuchanganya, huwezi kuwa *senior* kwa sababu shughuli ni hiyo hiyo ya ualimu ya taaluma ndiyo huyu mtu anaipata lakini kinachomuongezea sifa ni ule u-*senior* wake kwenye hiyo kazi, sasa kama siyo *experience* mimi nimeshindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama Serikali bado haitajibu naomba nitoe hoja tujadili ili ionekane wazi *seniority* ina tofauti gani na mtu kuwa na *experience* yaani hiyo *seniority* inatokana na kitu gani kwa sababu wote watakuwa na hiyo taaaluma ya utaalam.

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Hoja haikuungwa mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Jamani tunaendesha Bunge, hatuendeshi masuala ya nyumbani. *No,* Mheshimiwa Halima ngoja wewe unahesabu sasa hivi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ngojeni mimi nitakuwa *fair* ila kitu kimoja ambacho mna tatizo wakati wa kipindi cha Bunge hata wakati Waziri anajibu majibu sahihi kabisa mnakaa mna-*chat,* anapoanza kukaa mnarudia yale tena. Nilivyosema hoja imetolewa wamesimama watu saba tu, ngoja msitake kunibishia. Halima umeanza kuhesabu watu wakati ndiyo wameanza kusimama, *to be fair* nitaruhusu lakini natoa *warning* ya mwisho. Mpo Bungeni hampo katika ku-*chat* mambo yenu ya nyumbani na nitarekodi watu wote wanaotumia simu sasa hivi hapo maana ninawaona, sitawapa watu wote. Tunaanza na Mheshimiwa Ruth.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naunga mkono *issue* ambayo amei-*raise* Mheshimiwa Susan Lyimo, kwamba katika utumishi wa umma mtu anayekuwa *senior* ni mtu ambaye amefanya kazi kwa muda fulani kufuatana na ule muundo wa utumishi kwa sababu muundo wa utumishi unaainisha ni jinsi gani mtu anapoingia *entry point* anakuja anakuwa *junior, senior* na *principal.*

Kwa hiyo, *professionalism* ni zile *qualification* za hiyo kazi anayofanya ndiyo *professionalism* inapokuja. Moja kwa moja namuunga mkono kwa hiyo naomba hiyo *amendment* ifanyike. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo kwa sababu ni ukweli tunapozungumza *professionalism* huwezi ukauweka mbali uzoefu. Mara nyingi mambo mengine ya kitaaluma tunafundishwa na wote tuna-*graduate* pamoja lakini kinachotutofautisha ni uzoefu, mwenye uzoefu zaidi ukiongeza na ile taaluma yake ndiyo anakuwa *senior* zaidi kuliko yule mwenye utaalam ambaye hana uzoefu. Kwa hiyo, ni muhimu hiki kipengele kikaingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni jambo jepesi tu Serikali hebu wajaribu kukubali hili tuingize, hakuna utata hapa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *seniority* inaweza ikatokana na *qualification* za *profession.* Mtu anaweza kuwa ana miaka mingi kwenye kazi lakini *qualification* yake ikawa ya chini huwezi kumuita *senior* tu kwa sababu ya miaka mingi ya uzoefu wa kazi. Kwa hiyo, mtu anaweza kuingia kazini na *qualification* ya juu akawa *senior.* Kwa hiyo, naomba ibakie kama ilivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Dada yangu Susan, kwanza ni mzoefu

na ni mwalimu nashangaa anaweka kwamba uwe *professional* uwe umefanya kwa miaka kumi kitu ambacho uzoefu hata kwenye Bodi zingine ukishafanya mtihani na ukifaulu tu tayari unaitwa wewe ni *professional,* unaonekana ni *graduate professional. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii hoja ya Serikali ipo sahihi na hoja yake hafai kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan na *fact* yake ni ndogo tu kwamba unaweza uka-*qualify* kwa sifa za kitaaluma lakini ukakosa *experience* kwa sababu ndiyo maana tumeweka madaraja ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema kwamba hayo madaraja aliyasema ya walimu *TGTS* yanapanda kulingana na *experience* na miaka ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi sioni Serikali kwa nini wanaona ugumu kulikubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa muda na mimi niseme kwamba mambo mengi mazuri ameongea Mheshimiwa Susan lakini kwa hili simuungi mkono kwa sababu muda wa kukaa kazini au ujuzi siyo kitu pekee cha kumpa mtu utaalam au taaluma. Kuna mambo mengi ambayo yanaangaliwa ili kuona kwamba huyu mtu ni *professional. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna sababu ya *amendment* hii, kilicholetwa na Waziri kinatosheleza na ninaomba tuunge mkono kwa sababu kunaweza kuwa na mtu amekaa miaka ishirini lakini ukimuangalia ki-*profession*

yuko *weak* na kuna mwingine amekaa miaka mitano au sita yupo *strong* kwa *commitment* yake ya kufanya ile kazi.

Kwa hiyo, katika *profession* kuna ujuzi, taaluma, maadili *(ethics)* na kuna mambo mengi sana ambayo tunapaswa kuyaangalia.

Kwa hiyo, naomba tuunge mkono muswada ulivyoletwa na ili baadaye uwe sheria kuwe na haki katika kulinda na kuendeleza taaluma ya ualimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kikubwa tu sijui hapa kwa nini tunabishana sana, hata ukijaribu kuangalia uzoefu ndiyo kitu kikubwa zaidi kuliko jambo lolote kwa sababu hata wafanyakazi wote ambao wanapandishwa madaraja mbalimbali wanajaribu kuangalia hiyo ni sifa kubwa sana. Ninachoshangaa sijui kwa nini mnakwepa kwepa, hili jambo dogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila jambo tufanyie siasa, yapo mambo mengine ni mambo ya kukubaliana tu, tunakubaliana jambo linakwenda kwa sababu halibadilishi kitu chochote, lakini tunachotaka kuzungumza hapa tunataka kuweka kitu ambacho kitakuwa kinaonesha ni namna ni mtu gani anaweza kupandishwa na kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nashangaa tunabishana hapa, siasa hizi zitatupeleka wapi yaani kwa sababu tu ametoa Mheshimiwa Ruth Mollel basi, angetoa hoja hii upande wa huku tungesema sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hakuna anayeshangaa. Mheshimiwa Stella.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Lyimo lipo kwa mbali lakini naomba nitoe uzoefu kupitia Bodi ya Wahandisi ambayo mimi ni msajiliwa, ni *Professional Engineer PE 1656. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwanza hiyo miaka kumi tunayoizungumza ni mingi sana na mtu anapokuwa amemaliza, kwa mfano, amemaliza elimu yake katika ngazi fulani, inawezekana akakaa kazini na akafuatiliwa amefanya nini na huyo tayari akawa anatambuliwa katika ile taaluma. Kwa mfano kwa upande wa *engineers* ni miaka mitatu tu, sasa miaka kumi hiyo inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani ni vizuri mambo mengine kwa sababu hii bodi inahusisha kundi kubwa sana la Watanzania na kuna mambo mengi ya kuendelea kuyafanyia kazi. Hata kwa kuanzia pengine tunaweza kuchambua kupitia Kanuni kuliko kukimbilia kuweka hapa miaka kumi.

Mimi nashauri Mheshimiwa Lyimo ukubali ikae kama ilivyo ili ufanyike sasa uchambuzi mpana zaidi. *Engineers* tumefikia miaka 50 baada ya kuiboresha bodi hii kwa muda mrefu, kila wakati mnavyoanza mnaendelea kuiboresha. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka huko kwako hamna makocha wanafundisha mpira miaka 20 hawana vyeti, kwa sababu hawana *training?* Na sheria sasa hivi lazima uwe na *training* ya cheti cha *FIFA,* hata kama unafundisha kwa kutumia uganga lakini mpaka uende *training* ya *FIFA.* Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba siyo kwamba hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo haina msingi, isipokuwa je, ni wakati sahihi wa kuileta? Kwa sababu analeta neno jipya kwenye *definition* wakati haitumiki ndani ya muswada. Kama tunataka tuzungumzie kuhusu kuanza

kutengeneza *seniority* ya walimu inatakiwa huo mjadala utokee baada ya hapa, Serikali tuko tayari baada ya huo mjadala kufanyika ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha walimu wenyewe, baadae ndiyo twende tukalete kwenye kanuni au ikiwezekana huko mbele kuja kurekebisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tuchukulie mfano wa *Engineers' Registration Board. Engineers* wao wamejiwekea *categories* mbalimbali kwamba kuna *Graduate Engineer, Consulting Engineer,* kwa hiyo huko ndani wamejiwekea kwenye sheria yao lakini sasa kwenye sheria hii hatujaweka *categories* za Walimu kwa hiyo ukiweka kwenye *definition* haionekani kwenye Muswada kwa sababu haitumiki.

Kwa hiyo, tunaomba tulichukue kwa sasa tukaangalie kwenye kanuni baada ya kushirikisha walimu na wadau wengine ili tusilete mkanganyiko kwa sababu tayari kwenye utumishi wa umma kuna madaraja ya walimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, Serikali imeku-*offer* na *olive branch.*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri ananisikitisha sana. Huu muswada ni wa Wizara yake, anasema neno *senior* halipo, aangalie *section five,* aangalie *section 10,* naomba nisome, kwa hiyo, inaonesha kabisa Waziri au Wizara haijasoma huu muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu nataka Serikali watuambie huyo *senior* wanayemsema ana sifa zipi na ni kwa nini huku Bungeni tunasema Mheshimiwa Ndassa ni *Senior* au ni *Senator,* kwa nini Waziri Mkuu akiondoka hapewi Waziri mwingine anapewa Mheshimiwa Dkt. Mwinyi au Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe? *Why?* Hii ni kwa sababu wameandika wenyewe *senior* ndiyo sababu nilitaka tujiridhishe, huyu *senior* ni nani? *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Soma.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema hivi, naomba nirudie ili Waziri aelewe kwamba huu muswada labda hajausoma. Namba 5(1) inasema na nimerudia na nikasema kwa sababu hiki kipengele kimetumika kwenye 5(1) na 10 watupe *definition.* Inasema hivi; *A chairman who shall be appointed now by the President from amongst registered Senior Professional Teachers.* Ndiyo sababu nataka tuambiwe na ukija pia kweye *Registrar number 10,* inasema; *"The Minister shall appoint from the Public Service A Senior Professional Teacher."* Sasa hili neno ni wao wenyewe wamelitumia ndiyo sababu tunataka tupate *definition* hii *qualifications* zake ni zipi ndiyo sababu nikasema basi tuseme... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, nimekuelewa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenielewa, awe na *ten years.*

**MWENYEKITI:** Ndiyo nimekuelewa, sasa tunahoji Bunge, ndiyo taratibu zetu.

Waheshimiwa Wajumbe mimi ndiyo ninayesimamia shughuli hii.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Ndiyo ipi wameshinda?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Narekebisha. Waheshimiwa Wajumbe, mimi ni binadamu vilevile.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo imekataliwa, hoja ya Serikali ndiyo inayokwenda. Tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutupitisha haraka haraka, lakini siyo neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(a) nilitaka lile neno *chairman* kwa sababu masuala ya jinsia sasa hivi yamepamba moto na kwa sheria mbalimbali tumepitisha, neno *chairman* liondoke iwe *chairperson* ili ku-*promote both genders,* najua kwamba kisheria wanaweza wakasema *chairman* pia ni *chairwomen,* ina-*take both sex,* lakini nilidhani ikiwa *chairperson* inaleta maana zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeipokea na kuiona hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo, lakini katika utaratibu wa *drafting* ya sheria bado neno linalotumika ni *chairman* na siyo *chairperson* na hilo linatumika katika *drafting* mpaka sasa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivi, ninajua hilo analolisema lakini kwa muda mrefu hapa Bungeni tumekuwa tukibadilisha maneno na yamekuwa yakipita kama *chairperson* ili kuleta ile hoja nzima ya *gender.* Pamoja na suala zima la *drafting,* lakini mimi

naamini tumepitisha sheria nyingi tu na zilikuwa zinakubaliwa wakati wa *AG* mwingine. Sasa amesema ameikubali lakini sijui kama itabadilika au inabaki *chairman. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan lakini, ina *contentions* yoyote hii? Haina. Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno *chairperson* ni neno ambalo bado halijatambulika kwenye lugha ya kisheria, ni sawasawa. Kwa hiyo, kwenye sheria ukikuta *chairman* inamaanisha *gender* yoyote ile, ni sawasawa na neno *he,* bado inakuwa *interpreted* kwamba inamaanisha vilevile *she.* Kwa hiyo, kwenye lugha ya kisheria haina shida kuendelea kutumia *chairman* kwa sababu ndiyo imezoeleka na hata nchi zote duniani bado zinatumia neno *chairman,* ni lugha ya kisheria. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, hebu kubaliana na Serikali.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali, lakini mbona wewe unakataa? Kwa hiyo sawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan mabadiliko mengine.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namba 5; kwanza nashukuru kwa mara ya kwanza Serikali imechukua *amendments* zangu nyingi, lakini niseme tu kwenye hii sasa, jana wakati nachangia kuna ile *number four,* nashukuru kwamba wamechukua wale wa *private* na *public* kwamba wawe *nominated* na siyo Waziri ku-*appoint* kama nilivyokuwa nimeomba na kuweka kwenye mapendekezo yangu. Ile (v) ambayo ilikuwa (iv) sasa ambayo inasema *one representative appointed from among person with requisite qualifications to assist the board and to discharge of its funsctions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *members* wa bodi yoyote, ninavyojua na mimi nilikuwa *member* wa *board,* tunakuwa

na *status* ya kufanana kwa maana ya kwamba mnakwenda kufanya masuala ya maamuzi. Lakini nashangaa kwa nini huyu *particular person* anakuwa ni *more technical* wakati tuna sekretarieti ambayo ndiyo inapaswa kuwa na watu *technical* ambayo inapatikana kwenye *section 12.*

Sasa nataka kujua kwa nini hawa *members* Nane huyu mmoja yaani yeye atakuwa anafanya kazi nyingine ambazo ni *more technical.* Kwa hiyo, ninadhani nimeshindwa kuelewa, jana nilisema naona wamepunguza mmoja, walikuwa wawili, nikasema hawa wawili sasa wawe ndiyo wale walimu, wametoa mmoja, huyu mmoja bado wamembakiza anafanya kazi ambazo ni *technical,* sasa anakuwa kama ni *supporting staff* lakini hawa ni *board members*. Ninaomba maelezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba Mheshimiwa Susan Lyimo atuelekeze kwenye muswada anaposema huyu mmoja, ni yupi? Twende kwenye *section* ili iwe ni rahisi sisi kurejea na kukujibu.

**MWENYEKITI:** Ana-*refer part four.*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kabisa (v) sasa ambayo ilikuwa (iv) kutokana na marekebisho yenu.

Mimi nilikuwa nimeomba hawa watu wanaonekana ni *technical* kwa sababu mnasema awe na sifa *peculiar* ambazo zitasaidia *discharge of its functions* za *board.* Sasa nauliza kama huyu ni Mjumbe wa Bodi kwa nini huyu apewe *specific* kazi ambazo ni *technical* wakati *members* wa bodi kazi yao ni *decision making.* Sasa huyu kwa nini ni *technical* wakati kuna sekretarieti kule ambayo inafanya hizo kazi? Ndiyo swali langu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wale Wajumbe wote ambao wanatajwa Muswada unachopendekeza ni kwamba ukiacha wale ambao wametajwa *specifically* kwamba wanawakilisha taasisi au maeneo fulani, lakini kawaida ni utaratibu tu ambao tunautumia kumpa Waziri nafasi angalau ya kuweza kumteua mtu mmoja kwa ajili ya *competence* ambaye aaweza akahitaji kwa wakati fulani anapokuwa anafanya kazi. Kwa hiyo, inatoa *room* ya *flexibility* kwa Waziri kumpata mtu ambaye anamuhitaji ambaye wale watu wengine ambao wameletwa wanakuwa hawana hiyo sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano, kwa mfano kama *representatives* wengine ambao wameletwa ambao wanawakilisha taasisi labda hakuna mwanasheria, natoa mfano tu. Sasa ile kuweka mtu mwenye *requisite qualification* inampa nafasi Waziri kuweza kumleta mwanasheria kama anaona infaa kwa ajili ya uendeshaji wa hiyo bodi, ndiyo maelezo hasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo anachotaka kutuambia Naibu Waziri ni kwamba hii Bodi hawa Wajumbe hawana *qualification* kabisa isipokuwa huyo mmoja ambaye Waziri anamteua ndiyo anakwenda kufanya kazi. Sasa atuambie, hizi *qualifications* za huyu mmoja ni zipi kwa sababu mimi nilielewa kwamba kama anakwenda kusaidia bodi maana yake ukienda *section 12* kuna sekretarieti ambao hao ndio *technical people* ambao hii Bodi ni ya Waziri. Kwa hiyo hawa watu kama anataka yeyote Waziri ana Wakurugenzi kibao, ana watu kibao, kwa nini huyu mmoja tu kwenye bodi ambayo hii bodi kwanza kwa taarifa kawaida mi najua bodi inakutana walau mara nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu mtu ambaye ni Mjumbe wa Bodi kwa nini awe na *functions* mbili, yaani anakuwa kwenye bodi na huyu mtu kwa vyovyote atakuwa

na kazi nyingine kwa sababu hapa imeonesha kabisa kutakuwa na *lawyer,* kuna anayetoka sijui wapi na wapi, wataangalia vigezo hivi. Sasa huyu mmoja ndiyo atakayemsaidia Waziri hawa wengine hawamsaidii? Kwa hiyo mimi nimesema hivi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, *it's a very technical issue,* Serikali imejibu vizuri tu, kuna vitu vingine *technical* vinahitaji mtu awepo na aweze kusaidia. Ndiyo maana hata kwenye Bunge kuna Kanuni yetu, Spika au Kiti kinaruhusu mtaalam humu ndani asaidie ili aweze kujenga hoja, *it's a very clear matter,* kubaliana tu na Serikali twende.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja kwa sababu naona kuna mgongano sana hapo.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Haya, tunaanza na Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo, na kama hoja anayoisema Naibu Waziri kwamba wanahitaji ama Bodi inahitaji watu wenye utaalam maalum, ukisoma kifungu cha 5(4) kinasema hivi; "*The Board may co-opt any person with special knowledge or skills to provide expertise to the Board on general or specific issue but such person shall not have right to vote.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Susan ina mantiki kwa sababu bodi mbali na kuwa na sekretarieti, kama ambavyo imeanishwa na kifungu cha 12 na 13 ambao ni wataalam, lakini kifungu cha 5(4) kimetoa nafasi kwa bodi kualika mtu yeyote mwenye taaluma yoyote kutokana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ilikuwa tu ni *simple* kwamba *private sector* wanatengeneza asilimia 20 ya walimu wa nchi hii, kwa nini tutoe nafasi moja? Tutoe nafasi mbili ili waweze kuunganika na hili kundi kubwa ambalo Waziri analiteua. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan na Serikali ipokee, tusipende kubisha kila kitu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kupinga hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwa kusema kwamba kutakuwa na sekretarieti kwa maana kwamba kama Bodi itahitaji labda taaluma tofauti kwamba kutakuwepo na sekretarieti ambayo itaisaidia. Sekretarieti kazi yake ni kushauri, lakini Bodi ndiyo itakuwa inafanya maamuzi na ili kufanya maamuzi ni lazima kuwe na mchanganyiko wa taaluma mbalimbali. Ukiangalia ile namba tatu; *one representative nominated by the teachers' organization,* ndiyo kusema vyovyote huyu atakuwa mwalimu, *one representative from private sector,* huenda pia akawa mwalimu. Kwa hiyo, kutoa fursa kwa Waziri kuweza kuchagua mtu mwingine ambaye ataiwezesha Bodi kwa kuangalia majukumu mengine yanayofanywa na Bodi nadhani linapaswa kuungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga lile suala la Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware. Hukusimama? Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani jambo hili wala halina ugomvi mkubwa. Hoja hapa za msingi, nikimsikiliza Mheshimiwa Halima na Mheshimiwa Susan wanazijenga katika misingi ifuatayo; msingi

wa kwanza ni kwamba kuwe na *representation* ya labda wawakilishi wa walimu kutoka kwenye *private sector.* Sasa nikianza na hilo, ukienda kile kifungu cha nne tunachozungumza *two members appointed by the Minister* huwezi kujua labda *Minister* sasa atakapokuwa ana-*appoint* hapo unajuaje labda ataamua ku-*appoint* sasa kutoka kwenye *private sector?* Anaweza akaamua kwa sababu kwenye hiyo *private sector* ndiyo akapata zile *expertise* ambazo anafikiri kwamba zinakosekana kwenye Bodi, kwa hiyo hiyo anaweza aka-*consider* kutoka hapo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Subiri, utapata nafasi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anakosea...

**MWENYEKITI:** Utapata nafasi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Tayari ameshafanyiwa marekebisho, hicho anachosema siyo.

**MWENYEKITI:** Utapata nafasi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atapata nafasi. Lakini nirudi kusema, Mheshimiwa Halima amesema vizuri sana hapa, ameeleza hivi, kwamba kile kifungu cha 4 *co-option* ya *members* wengine ambao labda ni *expertise* nyingine kwenye Bodi tayari imekuwa *considered* kwenye kifungu kile cha nne, lakini tumemalizia pale hawana haki ya kupiga kura. Sasa kama hawana haki ya kupiga kura ina maana mjadala utakwenda, utakwisha watatoa ushauri wao, lakini kwenye kupiga kura labda jambo hilo linahitaji utaalam maalum, katika ku-*co-opt* wale watu ambao Waziri amewa-*nominate* na kuwaweka kwenye bodi, wenye utaalam watakaoweza kuisaidia bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba Mheshimiwa Waziri akiachiwa hili eneo anaweza akalitumia vizuri sana kuifanya Bodi iimarike na iwe na utalaam wa mchanganyiko wa kutosha wa kuweza kumsaidia na kuwasaidia walimu na timu nzima ya Bodi ambayo itakuwa inafanyakazi kwa niaba ya walimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, nimetoa mfano na nikasema mimi nilikuwa Mjumbe wa Bodi za Vyuo Vikuu. Kwa kweli Wajumbe wa Bodi wanatakiwa kazi yao iwe ni ya kutoa maamuzi, lakini wao wenyewe wengi wanakuwa na hizo *qualification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima amesema vizuri, kwamba kama ni suala la *technical* kuna hii *section four* ambayo inaruhusu. Huyu mtu yaani Mheshimiwa Jenista anakuja na hoja ya kwamba huyo atapiga kura, lakini kama ameshatoa ushauri wake, wale Wajumbe wanane wakapiga kura, hata wako *committed* wameelewa kwani hiyo kura itasaidia nini kama huyo ambaye unasema, inawezekana hata akawa anajua lakini akagoma kupigia kura hilo jambo alilolizungumza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala la kura wala halina msingi isipokuwa mi naendelea kusisita, na marekebisho yangu nilikuwa nimeomba hivi. Kwamba hicho kifungu kilichorekebishwa na Serikali bado nilikuwa naomba marekebisho yangu kwamba kwa sababu tunaingiza *private sector* na Serikali imekubali kumuweka mmoja hoja ilikuwa tuongeze mmoja kwa sababu ukiangalia hawa Wajumbe wengine wote ni Serikali angalia wa kwanza mpaka wa mwisho ni Serikali...

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Sasan umeeleweka.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja yangu ilikuwa ni hiyo nilikuwa naomba kama Serikali...

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo unaendelea na umekubaliana na upande wa Serikali?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** ...subiri basi! Hivi Halima hivi ukiwa Mahakamani pale wakili wewe Jaji una mu-*interrupt?* au unadharau tu humu ndani? *No! no! no!* ukiwa mahakamani wewe *were very good royal* ukiwa pale Mahakamani wakati Wakili anasema au jaji anasema na wewe unasisimama unasema yakwako? Mheshimiwa Susan umekubaliana na Serikali tunaendelea au.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata jibu la Serikali baada ya mimi kutoa maelezo yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serikali.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi namuomba Mheshimiwa Susan akubaliane na haya mapendekezo kwa sababu hiki kifungu au haya marekebisho yanalenga kuwa na mtu ambaye ana utaalamu maalum na anakuwa ni Mjumbe wa Bodi na anakuwa na haki ya ku-*vote.*

Hiki kifungu ambacho amekizungumzia, kifungu namba nne cha kusema kwamba Bodi ime i-*co-opt* uki m-*co-opt* mtu anakuwa siyo Mjumbe wa Bodi anakuja tu kwa ajili ya jambo mahsusi ambalo linajadiliwa siku hiyo. Hiki kifungu kinalenga kuimarisha Bodi. Naomba Mheshimiwa Susan tukubaliane tusonge mbele, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan kubali tu, kubali yaishe.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mi nadhani Profesa Joyce wangu mpenzi nadhani hatujaelewana, kwa sababu huyu mtu mmoja hawa watu wengine wote...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Susan haina haja ya mjadala.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme hivi sijakubaliana hoja yangu iko pale, naona...

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mimi naona unataka kunipeleka kwako.

**MWENYEKITI:** Hapana! Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Susan.

*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** *It goes without say*. Kwa hiyo hoja yako imeanguka, waliokubaliana na mapendekezo ya Serikali waseme ndiyo, kifungu hiki kinaafikiwa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa na mapendekezo kwenye *clause* 6(f) ambayo naona Serikali imeki-*delete,* kwa sababu kwa kweli tumepambana sana kwenye Kamati, lakini bado waling'ang'ania na nadhani walivyoona nimeleta wakaona sasa wakitoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yangu ya msingi ilikuwa hivi; kwamba ile (f) ambayo mimi nimeibadili kwa sababu niliona ina mapungufu makubwa Serikali ime i-*delete* lakini mimi nilikuwa nime i-*replace* kwa kuweka kile kifungu. Sasa kama Serikali itaona kinafaa ninasema kwamba (f) isomeke kwamba; kazi moja ya *function* ya hii Bodi itakuwa

ku-*promote teacher's quality through overseing training provided to teachers*. Kwa sababu lengo hapa ambalo ni *very crucial* kwa hii *professional* ya ualimu ni ubora wa mwalimu, tuone sasa kule kwenye vyuo walimu wanafundishwaje ili hawa walimu watoke sasa waende wakafundishe vizuri zaidi, lakini vile vile kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hayo yalikuwa mabadiliko yangu kifungu (f) kisomeke kama ifuatavyo; *"To promote teacher's quality through overseing traing provided by teachers"* kama itawapendeza. Nadhani hii ni *very crucial* kwa sababu ubora wa wawaalimu na kozi wanazofundisha au kufundishwa ni muhimu sana. Kwa hiyo kama Serikali ina hili la ubora wa wawalimu hawalitaki *then* tunaua elimu.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzisha hii Bodi si kuingilia vitu gani ambavyo vinafanyika shuleni. Hii ni Bodi ambayo kimsingi ina-*regulate* taaluma ya walimu. Hata hivyo katika *scope* ya majukumu yake, hata ukiangalia katika *functions* za hii Bodi haina mahali popote ambayo sasa inaanza kuingilia katika mafunzo ambayo yanatolewa kwa walimu. Kwa hiyo kifungu hiki kwa namna yoyote kile Bodi haitaweza kuingilia mafunzo yanayotolewa shuleni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sijasema kwamba kuingilia ila suala ni jinsi gani huyu mwalimu ataendeleza taaluma yake kama kule kwenye vyuo alivyosoma hakuna kozi zinafanana. Ukiangalia hata vifungu vingine kwa mfano (d) ambayo Serikali imeleta ndipo tutaona *contradictions,* anasema; *6.-(1)(d) promote, regulate and control continuing professional development for teachers*.

Haya yote pia yanahusiana na suala zima la maendeleo ya walimu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani huwezi kupima maendeleo ya walimu kama hujui kile

ambacho wanafundishwa; kwa hiyo ilikuwa ni ku-*oversee,* wala siyo kwenda ku-*oversee* siyo kuingilia. Sasa utajuaje huyu mwalimu wako utakuja kumdhibiti vipi kama hajafundisha vizuri kama kwenye kozi anazosoma Bodi haijawahi ku-*oversee.*

Mimi nilikuwa nadhani kuna hoja ya msingi kwamba lazima tuangalie pia kile kitu ambacho hawa walimu wanafundishwa kule kwenye Vyuo wanavyosoma, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Susan Serikali wamejibu *very professionally,* tena wamejibu kwamba hayo yakwako wameyachukuwa kwa lugha nyingine, wanasema *promote, regulate, controlling professional development for teachers.* Mheshimiwa Halima kakubali ya jirani yako hapo na wewe mwambie nini, umekubali?

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Wewe ndio mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri, maana yake mi nimeona Serikali imejibu vizuri tu hapa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimweleze Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba tulipoamua ku-*delete* kile kifungu ambacho ndiyo anasema turekebishe, kwa kweli tume-*delete* kwa sababu ya mapendekezo yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo kama anawasiwasi kwamba hatukutaka kuchukua *on board* kile alicholeta naomba nimpe *comfort,* kwamba tumekusikiliza wewe. Kwa nini tumekiondoa, ni kwa sababu baada ya kuangalia mapandekezo yako ni kweli kwamba ina utata fulani, lakini tayari kipengele cha 6(1)(a) ukikiangalia kwa ujumla wake kina *include* vitu vingine vingi ambavyo Waziri anaweza akapata ushauri kutoka kwenye Bodi kuhusiana na taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndio maana tumekiondoa kwa sababu kina utata lakini vilevile kwa

sababu umependekeza. Kwa hiyo tunaomba tuendelee kwa sababu *consign* yako tayari imeshachukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, nashukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nasema hata kifungu ulikuwa umesoma mwisho kabisa kikakuingia lakini ukaona, kifungu hicho kinaafikiwa na mapendekezo ya Serikali.

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lymo.

**MHE. SUSAN A. J. LYMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 14 nilikuwa na marekebisho kwamba hii kazi ambayo hoja hapa ya msingi ni *appointments* za Waziri ambazo zimezungumzwa; na ninashukuru kuna maeneo ambayo Waziri amepunguziwa hayo mamlaka. Hata hivyo ukiangalia hii ilikuwa inasema kwamba; *"14.-(1) The Minister may, in consultation with the Board and by notice published in the Gazette, appoint teachers to be supervisor..."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nadhani kwamba ni muhimu sana hawa watu ni wengi kwenye mikoa na Wilaya, nilikuwa nadhani kuna sababu ya hii kazi ikawa *published* wakafanya ikawa *competitive.* Watu hawa wakafanya *interview,* Bodi ikawasimamia *then* Bodi hapo baadaye ndipo ishauriane na Waziri, Waziri ateue kutokana na hawa watu wamefanya *all the interview* yaani iwe *competitive* na sio tu mtu amekaa ofisini anateua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi hoja yangu ilikuwa ni hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapendekeza tuendelee kubakia na kifungu kilichopo kwenye muswada kwa sababu hawa walimu ambao watakuwa *appointed* bado watabakia na vyeo vyao yaani si kwamba wanaacha majukumu yao yale ambayo wameajiriwa nayo.

Kwa hiyo ni *appointment* tu ya Waziri juu ya majukumu ambayo tayari wanayo kwa mujibu wa ajira yao, lakini vilevile ni kwa sababu ni suala la kiutendaji zaidi; kwa sababu Waziri anakuwa ana *appoint* watu ambao tayari wako chini yake. Kwa hiyo, ndio maana tunasema kwamba haina haja ya kufanya kwamba Bodi ndiyo iteue kwa sababu ni suala la kiutendaji na wale watu sio kwamba wanahamishwa nafasi wanabakia kuwa ni walimu kama walivyokuwa huko mwisho. Kwa hiyo ndio maana tunasema ibakie vilevile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba hoja ya Mheshimiwa Waziri ku-*appoint* ni kwa sababu hii ni suala la kiutendaji lakini kubwa zaidi ambalo nail-*underline* anasema kwamba hizi ni kwa sababu pia hawa watu wanaendelea na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hawa watu wanaendelea na kazi zao hata kama watafanyiwa *interview* bado wataendelea na kazi zao, kwa hiyo hiyo si hoja. Hoja yangu ni kwamba pamoja na kwamba pamoja na kwamba watu wana edelea na kazi zao lakini iwe *competitive,* Waziri ateue apate wale watu ambao ni *cream.* Pamoja na kwamba wanabaki kwenye kazi zao, lakini wawe wamepitia kwenye mchakato fulani, hawezi tu kusimama akasema fulani kwa sababu anatoka pale aingie.

Mimi nilikuwa nadhani hii kazi anaenda kufanya si ya uwalimu, anakwenda kufanya kazi ya *inquiring,* kwa sababu hawa watu ni wale wanaenda kufanya kazi ya kuweza kufanya masuala ya kuchunguza, hii inahusiana. Hawa *actually* ndio wa mwanzo kabisa ambao wanapelekea mwalimu kusimamishwa kazi au kufanyiwa chochete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nadhani lazima hawa watu wawe ni watu ambao wamepitia kwenye kamchakato fulani. Hatumnyimi Waziri ile kazi yake ya ku-*appoin*t au Bodi, lakini wawe wamepita kwenye mchakato ambacho ni *competitive* ili uweze kupata mtu ambaye kwa kweli huyu atamtendea haki huyu mtu ambaye baadae anakuja kufanya hiyo kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, hapa Waziri ana *consult* Bodi wewe unataka Bodi ifanye hiyo kazi peke yao; anayetumbuliwa hapa ni Waziri mambo yakiharibika. Kwa hiyo Waziri ana *consult* Bodi yake. Bodi inakaa inamwambia bwana fulani na fulani anafaa, Waziri anasikiliza Bodi *what is the problem* Susan. Mimi nimeingia tu Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Susan Lymo anaongea kitu kile kile ambacho kipo kwenye muswada kwa lugha nyingine yakwake yeye mwenyewe. Kwa sababu tunachosema ni kwamba Bodi yenyewe ndio inafanya mchakato yaani kama ni kuanza kuangalia kama nani anafaa ni Bodi.

Hata hivyo, kwa utaratibu tu wa kitaasisi Waziri ndio *appointing authority,* ni *machinery* hiyo hiyo moja anafanya kazi Bodi halafu Waziri ndio anaandika kwamba nimeku-*appoint* ndio utaratibu tu wa kawaida, kwa hiyo aina utofauti sana na unachokisema wewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan mambo mengi Serikali yameyakubali kwako ukiwa umetumia lugha nyingine ndio hayo hayo ya kwako.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mimi hoja yangu ni kweli kwamba Bodi, sasa kumekuwa na *confusion* kwa hiyo tunachokubaliana kwamba kutakuwa hiyo Bodi kwa vyovyote vile inasema kwamba Waziri ata-*consult* ndio baada ya wao kuwa wamefanya hiyo kazi ya kuwapata, *then its okay*.

**MWENYEKITI:** Sawa!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Haya.

**MWENYEKITI:** Jamani lugha ngumu hizi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadilko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara ilitajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha18(2) nimesema kiwe *deleted,* na sijajua kama kimekuwa *deleted,* hawaja-*delete*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ya msingi hiki kifungu kinazungumzia susla la *registration* na *qualification* zake *qualification for registration*. Ni jambo la kushangaza kwamba inasema; *18.-(2) The Minister, may upon consultation with the Board, make regulation prescribing additional qualifications or requirements for registration, as may consider necessary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linashangaza hizo *additional qualification* mimi kwangu naona ni tatizo kubwa sana, kwa sababu huwezi kuwa na *qualification* za *registration* halafu kuna nyingine umeziweka mfukoni unakuja kusubiri uje uziweke kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nadhani hakuna sababu lazima hizo *qualifications* zijulikane in *advance* ili watu waweze ku- *register.* Kwa sababu unaposema *additional* kweli ziko wapi hizo *additional* hawa kwa mfano mwalimu ame-*register* mwaka huu kwa *qualification* hizi halafu kuna walimu wanakuja ku-*register let's say two years to come* kunakuwa na *additional* nyingine, sasa wale si watakuwa wanatofautiana na wale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kusiwe na *proper standard registration qualification at the moment* ili walimu wote wawe na hizo *qualification* za *registration*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Susan wewe mwalimu tena mwalimu mzuri sana mimi hata *I don't see* kabisa hoja yako Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri anachopendekeza Mheshimiwa Susan Lyimo kina msingi kwa hiyo tunakubali ku-*delete*. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadilko yoyote)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifgnu hicho cha (21) ambacho sasa nadhani Serikali ilitoa ile (a) inakuwa (a) hiyo nilikuwa nasema hivi kifungu kilikuwa kinasema; *21.-(1)(b) has successfully completed an aproved course relating to teacher training",* yale mengine ya Serikali nimekata. Mimi nilikuwa nasema ibadilike iwe hivi; *"In order to be a registered teacher such person shall satisfy the body that he has successfully completed an approved teacher education course."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali inatuambia *course relating to teacher training.* Hii ina maana gani, hii *relating to teacher* inawezekana kabisa akawa sio mwalimu. Sasa mimi nilikuwa nadhani iwe ni *proper* kwa sababu tunahitaji walimu, tunataka walimu tunataka taaluma ya walimu hatutaki tena makanjanja kama wengi wanavyosema, unaposema *course* zinazo randana na uwalimu inawezekana isiwe uwalimu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani iwe *proper teacher* iwe ni *completed an*

*approved teacher education course.* Huyu awe amemaliza kozi za elimu na uwalimu, lakini ukisema tu *relating*, hii *relating* kwa kweli mimi imenileta shida sana kwa sababu mtu anaweza ikawa inarandana, ina-*relate* lakini sio *purely* ualimu. Kwa hiyo hoja yangu ilikuwa ni hiyo kama Serikali itaona inafaa.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana Serikali imekubali kuondoa hiyo *phrase,* tusikilizane, hiyo inayosema *under at least one year of full time teaching to the satisfaction of their board.* Kwa hiyo sisi tumei-*delete* hiyo *requirement* ya *one year.*

**MWENYEKITI:** Susan umekubali?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ilishatolewa na nimesema hayo maneno yote ya Serikali kuanzia *"and"* yametoka. Mimi hoja yangu ni *relating. Relating...*

**MWENYEKITI:** Yeye hoja yake *(b) complete and approve course relating to teachers training.*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Ndiyo, hiyo ndiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** ...ndiyo hoja yake.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mimi nimesema...*okay.*

**MWENYEKITI:** Anasema *relating* ina *corrupt training ya teaches,* yeye anataka *specific* ibaki *teachers training*. Serikali isi-*relate.*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la lugha, kwa hiyo ni suala aidha, Mheshimiwa Susan Lyimo ndiye mtaalam wa *drafting* au timu ya *AG,* lakini cha msingi tuko tayari kuangalia hiyo

lugha kwa sababu sidhani kama ni suala la *substance*, ni suala la lugha.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imefutwa)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa tu naomba ufafanuzi wa hiki kifungu cha 24 ambacho kinakuwa cha 23 sasa cha Serikali.

Wakati Naibu Waziri anatoa majibu alisema kwamba wamesikia kilio cha Wabunge kuhusiana na tozo mbalimbali ambazo walimu wanatozwa na kwamba watazipunguza. Sasa wamesema watazipunguza kimaneno, lakini sijaona popote palipopunguzwa.

Sasa nimejaribu kufuatilia, kwa mfano makato ya walimu peke yake, *PAYE* ni kati ya asilimia tisa mpaka 25 kutegemeana na mshahara, *Loans Board* asilimia 15, *PSPF* asilimia tano, *NHIF* asilimia tatu, CWT asilimia mbili. Kwa hiyo, unakuta kiujumla walimu wanakatwa siyo pungufu ya kati ya asilimia 40 hadi 50, ni makato peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa Waziri anasema kwamba itapelekea kwenye *regulation,* lakini wakati huo huo anasema imepunguzwa ili kupunguza mzigo. Sasa nilitaka tu Waziri anipe ufafanuzi husasani Naibu Waziri kwa sababu

ndiye aliyelieleza hili, huu mzigo wa ziada wa malipo ya *registration* na mzigo wa ziada wa malipo ya licence, kwa nini…

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Halima, umeeleweka vizuri sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** …nimeeleweka vizuri?

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, Serikali

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwanini msifute kama Wabunge walivyosema kwasababu mzigo wa walimu ni mkubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipokea hiyo hoja ya muswada au sheria itakayoanzishwa isijeikaleta mzigo kwa walimu kwa ajili ya kulipa *fees* mbalimbali ambazo si muhimu. Ukweli wa mambo, marekebisho ambayo tumefanya kwa kiasi kikubwa imeondoa *fees* ambazo zingelipwa kama ingepita kama ilivyo. Kwa mfano kwa sasa muswada ulivyo na baada ya kuleta marekebisho, usajili utakuwa ni wa mara moja tu, wakati huko nyuma ilikuwa usajili ni wa mara mbili na kila wakati ulikuwa unatakiwa ulipe *fee* ya usajili, lakini sasa hivi kuna *full registration* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile huko kwenye muswada ilikuwa ukisajiliwa lazima ulipie leseni, kwa sasa pale unapopata usajili haulipii leseni kwahiyo tumefanya kwamba unalipa *fee* moja wakati ulikuwa unalipa kama tatu pale mwanzoni. Lakini hata hivyo, viwango vya *fee* bado havitokei kwenye sheria, vitakwenda kuwekwa kwenye Kanuni na tunachoshauri tu ni kwamba, maamuzi ya kwamba ni kiasi gani kitalipwa, kitalipwa baada ya kufanya *consultation* na wadau wakiwepo walimu wenyewe. Kwa hiyo tumepunguza sana, lakini lazima tukumbuke kwamba bado kutakuwa na kulipa fee kwa sababu ile ni Bodi, lazima ijiendeshe lakini ilimradi isiwe kwa kiwango ambacho kitawaumiza walimu.

**MWENYEKITI:** Yah na Bodi inapokjea fee itakuwa inafanya *training* za walimu kutokana na *fee* zao hizo hizo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti marekebisho yangu ni madogo tu. Nilipendekeza kwamba yatoke haya maneno ambayo yanafuatia; *"person and subject"* ambayo yanasoma *"who does not satisfy the requirements under this section."*

**MWENYEKITI:** Kifungu kipi hebu kisome vizuri.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, au nikisome chote?

**MWENYEKITI:** Kisome chote.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Kinasema; 26.-(1) *"The board may grant provisional registration to a person who does not satisfy the requirements under this section, subject*

*to any conditions it consider the appropriate and if it is satisfy that..."* unaona kuna (a) na vifungu vyake vidogo vidogo na (b). Sasa nilikuwa napendekeza kati ya nena *"person"* na *"subject"* haya maneno *"who does not satisfy the requirements under this section"* yatoke

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapendekezo yangu ni kutokana na kwamba, ukiangalia hizi *requirements* ambazo zinasemwa *under this section* zinaonekana katika (a) na (b) ambazo ndizo zinazohitajika ili Bodi iweze kutoa hii *provisional registration*. Sasa tukiacha haya maneno yakaendelea kuwepo ni *contradiction,* na pengine nilifikiria labda Serikali inaweza kuleta marekebisho, kwamba labda *conditions* hizi ni za 25(1) ambayo inakuwa 24(1). Kama itasema kwamba ni *conditions* katika 24(1) tuiache hiyo sentensi, lakini la sivyo ni bora tukaitoa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Wambura tunafikiri yale ambayo anapendekeza yana msingi, kwa hiyo, tunakubali kuyaondoa hayo maneno.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuko Bungeni, ndiyo na siyo ziwe kwa sauti. Mnazungumza sana, mnajibu kama vile

mnavyopenda hatuendi hivyo jamani. Pande zote mbili ukikubali ndiyo, ukikataa siyo kwa sauti. Hili ni onyo la mwisho kwa Bunge zima, acheni mazungumzo, sikilizeni muswada.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mnaambiwa huko sikilizeni muswada.

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mapendekezo kwenye kifungu hiki kwa sababu ukiangalia kifungu hiki cha 37 kiko *related* na kifungu namba *35/section 35* ambapo ukiangalia pale kuna kumuondoa mtu kwenye *register* au kwenye usajili na wametoa maelezo pale kwenye 35. Hata hivyo ukija kwenye adhabu kuna makosa ya aina mbili tofauti, kuna yale ya kuwa *reinstated* kama

labda ameghushi vyeti au amepoteza na nini, lakini kuna ile kutokulipa *fee* sasa pale alikuwa amechanganya hizi adhabu na mimi ndipo nikaona kwamba tuongeze kifungu cha tatu kitakachosomeka; *"Person to sub-section (2) defaults relating to profession academic qualification shall attract sitting for examination and those relating to other reasons including fee payment shall attract penalty."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali pamoja na marekebisho yao pamoja na kwamba wameingiza haya ya kwangu, lakini nilikuwa nadhani bado haijakaa ninavyoiona mimi. Anasema; ***"and certainty with the pay or pays a penalty fee may be determined by the board."***

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nadhani kuna vitu viwili hapa, kuna ile mtu kwa mfano, amefeli kulipa *prescribed fees* yeye ikabidi alipe *fee penalty,* lakini kuna wale ambao wamekutwa labda na *forgery* ya vyeti na nini hao nao watakuwa na adhabu yao tofauti. Kwa hiyo nikadhani tuongeze kifungu cha ttau ambacho kitakuwa kina-*qualify* kile kifungu cha pili kama *drafting* kwa *AG* au Mawaziri wataona inafaa, nilikuwa nadhani ilivyokaa inaleta *confusion,* lakini ikiwa *separated* mtu atajua kwamba nikiwa na kosa hili la *academics then* nitafanya mitihani lakini nikiwa na makosa haya mengine yanayohitaji *penalty and what* itakuwa na adhabu hiyo. Kwa hiyo nilikuwa nadhani hizi adhabu mbili zitenganishwe.

**MWENYEKITI:** Yeye ameongeza kifungu kingine kukifungua zaidi. Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo akisoma hicho kifungu cha 37 pamoja na cha 36 ataelewa lengo la marekebisho ambayo tumeyaleta. Kimsingi tunachosema ni kwamba pale mwalimu atakapokuwa amefutiwa leseni kwa sababu yoyote ile maana yake kuna kipindi atakuwa nje ya *practice*, atakuwa nje ya kazi. Kwa hiyo, lengo la kutakiwa afanye mtihani ni kwa kumuangalia kama bado ana-*qualify,* au tuseme bado anaweza kufundisha.

Kwa hiyo, lengo la mtihani siyo kumuadhibu, lengo ni kum-*assess* kama baada ya kuwepo nje ya mtihani bado ana zile *competence* kama mwalimu? Kwa hiyo, hapa tukisema kulipa *fine* maana yake bado tutakuwa tumemueondolea jukumu lile sasa la kuonyesha kwamba bado ana *competences.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya hivyo ni ili Mwalimu ambae ameondika nje ya ufundishaji kwa muda ni ili tuweze kumrudisha lakini baada ya kujiridhisha kwamba bado anafahamu kazi ya ualimu. Kwa hiyo, tunapendekeza ibaki kama tulivyopendekeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama tumeelewana na Naibu Waziri. Ukisoma huu muswada toka mwanzo halafu nisome na haya marekebisho ya Serikali na yangu halafu tutafanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni ilikuwa inasomeka hivi; 36.-(2) A *person who fails to submit an application for the statement of his registration, within the period stipulated under the provisions of sub-section (1)...*ambayo hiyo *sub section (1)* ndiyo hiyo inatokana na ile *section (35)* ambayo ni *removal of the name from register,* inasema kwamba...*"shall not be reinstated unless he passes an examination or pays a penalty fee as may be determined by the board."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali imeleta marekebisho ikisema kwamba wataondoa ile 35, sawa, 36 imefutwa lakini *deleting the words or pays a penalty as may be determined by the board.* Kwa hiyo ina maana inabaki tu *passes an axamination.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwamba kwa mfano, kama huyu mtu amepoteza, ukiangalia zile (a), (b), (c), (d) zote pale kuna ambazo hazihusiani na cheti au na nini, sasa hii *penalty* inalipwa kwa kitu gani? Kwa hiyo,

nilikuwa nafikiri *examination* i-*deal* na… *unless* mnatuambia kwamba haya makosa yote haya yaliyotajwa kwenye *sub-section 35 penalty* yake ni kufanya mitihani. Kwa maana ya kwamba mtu akiwa *engaged* kwenye *forgery, mis-representation, fraud conduct and* nini anafanya *examination, is it so?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi hoja yangu ilikuwa ni hiyo, kwamba kuna makosa ambayo hayaendani kabisa na kufanya mtihani. Angalia kwa sababu kama haya mna-*relate,* na Mheshimiwa *AG* naomba usaidie hapo, kwamba kama haya makosa yako *related* na kifungu cha 35 ambacho ninyi wenyewe kwenye marekebisho yenu mmekieleza sasa adhabu zake ni zipi? Ndiyo sababu nikasema hizi adhabu zinapaswa kuwa mbili tofauti. Kuna zile ambazo zinatokana na *qualification* amepoteza cheti, amefanyaje, afanye mitihani, lakini haya mengine yanahitaji *punishment* ya jinai, yanahitaji *penalty,* ndiyo hiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan umesoma marekebisho ya Serikali? Soma *clause 37* inasema nini? Wanasema Serikali *"deleting the words "or pay in penalty fee as may be determined by the board appearing in sub-clause"* wao Serikali wamefuta.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, hujanielewa, ni kwamba soma ile *section 37* inavyoanza inasema, na wamerekebisha wenyewe, wametoa ile 36 ikawa 35. Ukisoma 35 pale juu angalia; 34.- *The board may cancel or suspend the name of a person from the register if such person-*

*(a) fail to pay the prescribed fees"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza kama amefeli *prescribe fee* kulipa, anakwenda kufanya mtihani au atadaiwa hela, *penalty?* Ndilo swali.

**MWENYEKITI:** Serikali mmeilewa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naoimba nizungumze kwa utaratibu sana. Kifungu cha 36 twende kwanza kwenye hicho, kinazungumzia kuhusu ku-*cancel registration* (kufutiwa usajili kama mwalimu) maana yake mwalimu anakuwa amefanya makosa ambayo yanafanya Bodi iweze kumfutia usajili. Sasa tukamfutia. Kifungu cha 37 ni kwamba baada ya kufutiwa anaweza kuomba tena baada ya muda fulani asajiliwe tena au apate tena leseni ya kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo tuliyoleta ni kwamba kama mtu amekuwa nje ya ufundishaji, nje ya kazi kwa muda fulani tuseme miaka mitatu maana yake ile taaluma yake ameshaanza kuisahau sahau na ndiyo maana tunapendekeza tunampa mtihani. Sasa kwa nini tumeondoa *fine?* Ni kwa sababu *fine* hapo haisaidiii chochote kwa sababu lengo letu ni *profession*, ni kutaka kumuonesha huyu mtu kama badi yuko *active,* bado ana kumbukumbu na ndiyo maana tumebakiza mtihani tu. Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema ibakie hivyo hivyo sasa sijui tunashindwa kuelewa nini!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan. Serikali imejieleza vizuri tu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Nawaambia hizi lugha zilizoletwa na meli ni taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi adhabu zinatokana na kifungu cha 35, Waziri tuko sawa sawa? Ndiyo sababu nauliza kwa mfano, kama amefanya kosa lifuatalo; ame-*forge,* amefanya mis-*representation,* amefanya *fraudulent conduct,* ame-*fail* ku-*pay prescribe fee,* huyu mtu anatakiwa afanye mtihani au anatakiwa ashitakiwe kijinai au alipe *fine?*

Mimi hapo ndiyo sija...,hebu niambieni kwasbabu hizi adhabu naomba na wewe hebu soma hiki kifungu cha 35 ambacho ndiyo hicho Serikali imerekebisha hapa.

**MWENYEKITI:** Wamekuelewa, Mheshimiwa Profesa

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Rafiki yangu Susan usikasirike basi.

Mimi niseme tu kwamba hapa anachokisema Mheshimiwa Susan Lyimo tunamuelewa vizuri, lakini labda yeye anachoshindwa kuelewa upande wa Serikali hiki kifungu ni matokeo ya hivyo vitu ambavyo umevifanya kwamba vikasababisha ukafutiwa usajili, aidha, umefutiwa usajili kwa kutokulipa ada au umefutiwa usajili kwa kughushi au umefutiwa usajili kwa sababu yoyote ukakaa nje ya *profession* kwa muda ambao utaelezwa katika sheria hii, hutaruhisiwa kuingia darasani kufundisha kama umekaa nje muda mrefu mpaka upewe mtihani kujiridhisha kwamba kukaa kwako nje bado *network* yako inafanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu aunge mkono tusonge mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan tumalize. Limeeleweka vizuri tu hilo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani wamenielewa kama alivyosema Profesa na *AG* namuona anacheka nadhani watakwenda kufanya marekebisho walete kwa sababu hiki kifungu ni *confusion* tupu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba Serikali imechukua mapendekezo yangu kwa sababu lilikuwa ni jambo la kudhalilisha sana walimu. Haiwezekani walimu kwa sababu hiyo ndogo tu ameondolewa, amefanyaje aende akazungushwe mpaka vijiji vyote waone, nashukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa hiyo nime *drop* ya kwangu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 42

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali imechukua mapendekezo yako kwa hiyo nashukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati yaBunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57

*(Ibara ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 60
Ibara ya 61

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 70

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote).*

Ibara ya 71

*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

Ibara ya 72

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 73

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 74

Ibara ya 75
Ibara ya 76

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG.LINAH KITOSI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae, mtoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1)ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la mwaka 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa ya Bodi ya Kitalaam ya Walimu Tanzania ya mwaka 2018 *(The Teachers Professional Board Bill, 2018*) kama ulivyorekebisha katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mweyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuanzishwa Bodi ya Kitalaam ya Walimu Tanzania kwa lengo la kuinua kiwango cha taaluma ya ualimu na kupata walimu mahiri, kuanzisha

mfumo wa usajili wa walimu, kutoa leseni za kufundisha kwa walimu na kuweka vigezo na viwango pamoja na mambo yanahusiana na hayo *(A bill of an Act to establish the Tanzania Teachers Professional Board, to deal with professional competence and practice, maintenance of register of professional teachers and to issue license for practice teaching, maintenance and establishment of teachers' professional standard and conduct and to provide for other related matters)*.

*(Kusoma Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sheria imeshasomwa mara tatu na sasa ni sheria rasmi ya Bunge. Kwa hatua yetu sasa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:**...Mwakajoka unajua heshima ni kitu cha kawaida sana. Nasema na Haonga vilevile nimekusikia. Waheshimiwa mnajua hatufanyi mchezo humu ndani, naweza kumtoa mtu hapa asirudi mpaka kiama hapa. Ukitoka hapa na huko unaharibikiwa vilevile. *(Makofi/ Kicheko)*

Kwa hiyo, sheria hii imepita, nawapongeza sana Serikali. Waziri, Naibu Waziri na AG, *Chief Whip* na upande wa Serikali na Wabunge wote wa pande zote mbili, pamoja na Mheshimiwa Susan mapendekezo yako mengi yamekubaliwa na Serikali, imeonekana namna Serikali ilivyo sikivu, kwa hiyo, mambo mengine madogo madogo acheni, Gekul uwe na nidhamu. *(Makofi)*

Sasa naagiza Wabunge wote ambao bado wana miswada haijakamilika warudi kwenye Kamati zao wakahakikishe miswada inakamilika na inakwisha siku Ijumaa wakati tunafunga Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nawatakia kila la heri, naahirishwa shughili za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7:00 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa Tarehe 7 Septemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*